Muhuri Ya Mungu

. . .-fufuo, ule wa mtindo wa kale tu tuliozoea kuwa nao miaka mingi iliyopita, nasi tunafurahia jambo hilo sana. Nami nafurahia kuimba huku kwingine, na kuimba kwote, na hizi nyimbo maalumu. "Nimesafiri maili ya mwisho ya hiyo njia; nitapumzika mwisho wa siku." Hapo ndipo ambapo, labda, nikiketi tu hapa, wakati walipokuwa wanauimba, nikiangalia nje na kuona jua likitua; ndege wote wakiimba kwa sauti ndogo na nyororo, yote karibu yamekwisha sasa nao wameenda kupumzika, kesho asubuhi wapate kuamka kwa ajili ya siku mpya.

2 Basi hivyo ndivyo ilivyo na maisha; siku za kufanya kazi hatimaye hupita, nasi tunalala kitandani. Ningependa kuzungumza Naye siku hiyo, kuzungumza Naye tu. Nijifunike nguo zangu, niingie kwenye kile chumba.

3 Nikijua jambo hili, kama Mtakatifu Paulo alivyosema, "Ninamjua katika Nguvu za Kufufuka Kwake." Ili kwamba, atakapoita kutoka katika wafu, nitaitwa pamoja nao. "Nikimjua katika Nguvu za Ufufuo Wake." Si kumjua kwa neno wala kwa tendo, bali kumjua Yeye katika Nguvu za Kufufuka Kwake. Hayo ndiyo matumaini ye—yetu makuu usiku wa leo, na tumaini pekee tulilo nalo, ni katika . . . kule kufufuka kukuu kwa Bwana wetu Yesu; na ule utangulizi wa ufufuo tulio nao sasa, kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa kuwa na Uzima wa Milele katika Kristo Yesu.

4 Tukingojea, na kule kungoja kutukufa, kwa maumbile yote, hata siku ile atakayokuja mara ya pili, kutoka Mbinguni, Yeye ambaye Mungu atamtuma katika wakati ufaao. Nayo miili hii ipatikanayo na mauti, tunayougulia itachukua kutopatikana na mauti, "Nasi tutabadilishwa kufanana na mwili Wake ulio mtukufu, kwa kuwa tutamwona kama alivyo."

> Ndipo dhambi na huzuni, dhambi na mauti ya
> ulimwengu huu wenye giza vitakoma,
> Katika utawala huu mtukufu pamoja na Yesu
> miaka elfu moja ya amani.

5 Ndege wanangojea wakati huo. Miti inangojea wakati huo. Maumbile yote yanainama na kulia, yakingojea wakati huo, yakiugua yapate kuvikwa nguo.

6 Msichana wangu mdogo, muda kidogo uliopita, aliniuliza swali. Akasema, "Baba, ulimwengu huu ulionekanaje wakati Mungu alipoumaliza?"

7 Nikasema, "Ulikuwa mzuri, kipenzi. Ulikuwa mzuri." Kisha nikasema, "Siku moja utakuwa namna hiyo tena, wakati laana

itakapoondolewa. Kisha tuta...Utakuwa kama ulivyokuwa hapo mwanzo, bustani kuu ya Mungu."

8 Naam, tuingilie kazi mara moja. Nilikuwa nikiwazia sasa, usiku wa kwanza...Huu ndio usiku wa tatu wa ufufuo wetu mdogo. Nasi hatujakuwa na kampeni ya uponyaji. Ni kustarehe tu, kuonyesha tu tunavyojisikia, na kufundisha Injili katika njia ya mtindo wa kale; Injili ile ile niliyofundisha hapa, mika mingi, mingi sana iliyopita, sijabadilisha hata kidogo. Hiyo ni kweli, Injili ile ile tu, sijaifanya upya wala kuipiga msasa hata kidogo; ni Injili ile ile tu.

9 Huko nje katika ibada, zikiwa za madhehebu mbalimbali, kwa kuwa zinafanyiwa katika vyumba vya mikutano na madhehebu mengi mbalimbali ya watu wakija pamoja, kwa namna fulani unajizuia mwenyewe kutokana na Fundisho; yote ila kuponya Kiungu, na, bila shaka, kumkubali Bwana Yesu. Bali unapokuwa nyumbani mwako, kama vile kanisa la nyumbani hapa, unajisikia kama kwamba utatoa tu ukosi wako, na kuhubiri vile tu unafikiri ni kweli, na jambo ndilo hilo.

10 Na wakati mwingi, katika mahali hapa, tuna, mara nyingi, watu hawakubaliani. Hatuwezi kutarajia kila mtu akubaliane nasi juu ya Mafundisho ya kanisa letu na mambo tuliyo nayo. Lakini sisi tunge...labda ni jambo lile lile, kama mchungaji wako alikuwa anahubiri, bali angekuwa angali ndugu yangu. Kwa hivyo usijali jambo hilo. Na kila mtu huangalia mambo katika mtazamo tofauti.

11 Basi katika juma hili, kwa kuwa ilinibidi kufutilia mbali juma moja huko Canada, kwa sababu ya tufani ya theluji, naam, ilinipa majaliwa ya kuweza kuja hapa kwenye maskani kwa ajili ya ufufuo wa siku chache usiku, ambao niliahidi nilipoondoka. Nami nilitangaza, ya kwamba hakukuweko... "si ibada ya kuponya; ni kuhubiri tu Injili." Ninino tu...Na juu ya jambo hili, kupata, nilidhani labda tutachukua siku chache usiku juu ya Nyakati Saba za Kanisa. Kwa maana kweli ninaamini ya kwamba tunaishi katika wakati wa mwisho wa kanisa, siku ya mwisho, kabla tu ya Kuja kwa Bwana Yesu.

12 Daima ninajaribu kujipima mwenyewe, kanisa dogo hapa, kila mahali ambapo nimekuwa nikizungumza, kwa kuwa Bwana mwema wa Mbinguni amenipa huduma dogo, pia, kwa upande wa ya kimbinguni, kama mnavyofahamu. Nao watu wanalishikilia neno lako, na—na kwa hiyo si—sina budi kuwa mwangalifu sana ni matamshi gani ninayofanya. Maana, kama Roho Mtakatifu amejalia nguvu hizi za ono na kutambua, ambazo ni halisi, nao wanakusikia ukizungumza, wao wanaona kwamba wewe una ufahamu wa yale unayozungumzia, la sivyo Mungu asingebariki kosa na kulipeleka nje namna hiyo. Mnaona? Kwa hiyo huna budi kuwa mwangalifu sana, na kulipima katika nuru ya Neno, wakati wote. Na katika jambo

hilo, kama nikifanya kosa, naomba Mungu anisamehe, maana simaanishi kufanya hivyo. Nami . . .

13 Basi wakati wo wote, katika kufundisha, na hasa katika masomo haya yenye kilindi tuliyomo sasa, na usiku wa jana juu ya *Alama Ya Mnyama*, na masomo kama hayo, na usiku wa leo juu ya *Muhuri Ya Mungu*, alama ya Mungu, na kadhalika namna hiyo, ninajisikia ya kwamba labda, huenda nikawa na wengi wasingalikubaliana na jambo hili, na yale ninayofundisha juu ya jambo hilo. Bali mimi hujaribu kufanya jambo hilo kama tu . . . si kulielekeza kwenye kanisa lo lote, madhehebu yo yote, wala watu wo wote, sivyo kamwe. Mungu anajua jambo hilo. Ni katika tu Nuru ninayoliona, hivyo ndivyo ninavyolinena.

14 Na hakuna kanisa ambalo linalitaja Jina la Bwana Yesu ila lile ningelipenda. Huyo si mtu ambaye angeweza Jina Lake, ama aliye na heshima yo yote Kwake, ila yule ambaye ningefikia kifo changu kuwafanyia jambo lo lote. Hiyo ni kweli. Haidhuru wanavalia mtindo gani wa dini, au ni Methodisti, Batisti, Katoliki, wo wote ule, hilo halingejalisha hata wakia moja kwangu. Hiyo ni kweli. Mradi tu wao wanamheshimu Bwana wangu.

15 Lakini, sasa, kuna Ramani. Na sasa kila kanisa linafundisha, labda, theolojia ya kanisa hilo ilivyo, wakiamini ya kwamba ina msingi wake katika ramani fulani. Vema, sasa, mara nyingi, katika kuona mambo hayo, hivyo sivyo tu ninavyoisoma ile Ramani, kwa hiyo basi nina haki katika kanisa langu mwenyewe kufafanua kile ninachofikiri ni kweli.

16 Hapa hivi majuzi, kondrakta . . . Nilikuwa huko Milltown, kwenye kanisa la Kibatisti huko Milltown, ambapo tulikuwa na ufufuo. Basi Ndugu Wright nanyi nyote, nafikiri, mnamkumbuka Marion Lee. [Ndugu George Wright anasema, "Amina."—Mh.] Naye alikuwa amefadhaika sana juu ya jambo fulani nililofundisha juu ya ubatizo wa maji. Vema, akaenda nyumbani, naye alikuwa amefadhaishwa na jambo hilo. Naye alikuwa ni kondrakta.

17 Usiku huo akaota ndoto. Bwana alimwonyesha alikuwa anajenga nyumba, naye alikuwa aweke dirisha linalotokeza mle. Na kwa hiyo badala ya kuweka dirisha linalotokeza mle, yeye aliweka tu ukumbi, kasema, "Hilo litakuwa sawa." Kwa hiyo mwenye nyumba alipokuja, kasema, "Ibomoe mpaka kwenye msingi; ukaanze tena."

18 Kwa hiyo yeye alikuwa amefundishwa jambo fulani mbali na yale Biblia ilifundisha, kwa hiyo akasema, "Afadhali basi niibomoe mpaka kwenye msingi na kuinjenga tena." Nilienda nyumbani pamoja naye usiku huo, tukakaa usiku kucha nyumbani mwake. Kwa hiyo basi sisi . . .

19 Hiyo ni kweli. Hauna budi kuwekwa. Na, nikifundisha masomo haya, mimi si mwalimu. Bali ninalojua juu Yake,

ninapenda kuwaelezea wengine, na kushiriki kwenye Neno, huku Roho Mtakatifu akilifanya dhahiri moyoni mwetu. Na kwa hiyo tunakuwa tu na wakati mkuu tukifanya jambo hilo.

20 Na kwa namna fulani kumpumzisha mchungaji wetu mpendwa hapa, Ndugu Neville. Kama kuna wageni malangoni mwetu; huyu mtu, *hapa*, ndiye mchungaji wetu, Ndugu Neville, mtu wa Mungu, mtumishi wa kweli wa Bwana Yesu Kristo. Sisemi jambo hilo kwa maana yeye ameketi hapa. Mimi husema hivyo asipokuwepo, ama mahali po pote, yeye amekuna namna hiyo tangu nilipomjua. Yeye alikuwa Mmethodisti kwelikweli, nami nilikuwa Mbatisti kwelikweli, bali tulikuwa ndugu pamoja, na kwa hiyo sote wawili ikatokea kwamba ni watakatifu wanaofingirika. Vema, sivyo, ndugu? Amina. [Ndugu Neville anasema, "Amina. Haleluya!"—Mh.] Kwa hiyo tuna msimamo wa pamoja.

21 Vema, sisi, tuna wakati wa ajabu kwa njia hii, "Tukiwa na ushirika tu mmoja kwa mwingine, huku Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatusafisha na uovu wote." Kwa hiyo tuna wakati mkuu, na bila shaka tunawathamini wageni malangoni mwetu, usiku huu, hapa.

22 Ufufuo wetu mdogo, nafikiri mnashangaa mbona haukutangazwa. Vema, ilikuwa tu ni wakati mdogo wa sikukuu kwa ajili ya kanisa letu hapa, na hiyo ndiyo sababu labda huenda ikawa . . . Sijui jinsi Roho Mtakatifu atakavyoongoza, lakini labda usiku mmoja, kabla hatujafunga hapa, huenda tukawa na ibada ya kuponya, Bwana akipenda. Na kwa hiyo ninatumaini ya kwamba atajalia jambo hilo.

23 Sina budi kurudi Canada sasa, kuendeleza ufufuo. Na kama wote wajuavyo, tuna orodha kubwa ya mikutano, imejazwa mpaka kwenye ile tarehe ya kwenda katika nchi za ng'ambo. Na mipango imefanywa tayari, kuanzia huko Durban, Kusini . . . katika Johannesburg, Afrika Kusini, katika Septemba, yapata tarehe tatu. Kisha tutaondoka huko tuingie Durban; hadi India; kisha Palestina; na Luxenburg; na Frankfurt; na Transjordan; na kupitia kule kwote. Tutarudi nyumbani wakati Bwana atakapotuongoza kurudi, atakapotuambia turudi. Kisha wao wanatayarisha utaratibu mwingine wa safari ya kwenda New Zealand na Australia, na kote kote chini kule; mpaka kuingia mashariki, hadi Japan, na nchi hizo zote kule.

24 Ninajisikia ya kwamba makanisa mengi sana karibu na hapa, ambapo watu, lo, jamani, wanaongoana wao kwa wao tu, na, halafu, maelfu ya watu hata hawajasikia habari za Yesu mara ya kwanza. Na kwa hiyo ninaona ya kwamba . . . Ni maoni yangu, binafsi, ni wajibu wangu kuupeleka Ujumbe kwao, vizuri niwezayo. Na sasa wakati ninapo- . . .

25 Hebu niseme tena sasa, maana, walioko, Methoditi, Batisti, Katoliki, Presbiteri, Pentekoste, Pilgrim Holiness, Nazarayo,

wameketi hapa, na hivyo ndivyo tulivyofanywa . . . Ninaamini hivyo ndivyo itakavyokuwa Mbinguni, kwa namn fulani, kundi letu lote limekaa kule.

26 Na sasa juu ya jumbe hizi, kama vile *Alama Ya Mnyama*, na leo wakati kuna mchafuko mkubwa hivyo . . . Je! mliufahamu huo, jana usiku? Kama mliufahamu, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa tutazungumzia usiku huu juu ya alama ya Mungu, ama, *Muhuri Ya Mungu*. Sasa tunatambua . . .

27 Naam, sijaribu tu kuhubiri kutoka katika Biblia mbili; moja yatosha. Bali nina moja hapa kwa ajili ya maelezo yaliyoandikwa chini ya ukurasa, na kadhalika, ya marejeo, kama mtu fulani angeuliza swali. Na sasa, kesho usiku, Bwana akipenda, baada ya kuhubiri . . .

28 Usiku wa kwanza, juu ya *Nyakati Saba Za Kanisa* kuona mahali tulipokuwa, tuko, mahali petu, katika siku tunayoishi.

29 Usiku wa jana, juu ya mhalifu mkubwa sana aliyeko ulimwenguni, *Alama Ya Mnyama*.

30 Halafu, usiku huu, juu ya baraka kuu sana zilizoko ulimwenguni, *Muhuri Ya Mungu*.

31 Kesho usiku, nitawapa nafasi kuniuliza, sasa. Kesho usiku ni maswali, na mambo ambayo hamfahamu kuhusu yale yamekwisha kuhubiriwa. Mmekuwa waungwana na mabibi kutosha, ama Mkristo kutosha, ningesema, kutulia kwenye wakati wa ibada. Ninawataka mliandike, kesho usiku mtakapokuja kanisani, na mje mapema tu mwezavyo, maana itanibii kuja mapema kusoma na kwa namna fulani kujibu, jinsi swali lenu lilivyo kuhusu Maandiko.

Halafu Jumapili asubuni ni shule ya kawaida ya Jumapili.

32 Jumapili jioni, labda Jumapili jioni, ni ibada ya ubatizo. Kuna watu watakaobatizwa. Halafu Jumapili usiku, labda sisi, au tutakuwa na ujumbe wa Injili ama ibada ya kuponya. Tutaona cho chote Bwana atakachotuongoza kwa ajili ya usiku huo, kwa ajili ya Jumapili usiku, ujumbe juu ya jambo hilo.

33 Sasa tunaona, kabla hatujakaribia jambo hili, ya kwamba, "Hakuna mtu Mbinguni, hakuna mtu aliyekuwa duniani, wala hakuna mtu chini ya nchi, aliyestahili kukichukua kile Kitabu, wala kukifungua, wala kuzifungua Muhuri zake." "Hakuna mtu!" Yohana aliona jambo hilo katika Ufunuo. Nasi tunafundisha Ufunuo sasa. "Kisha Yohana akalia. Lakini kulikuwa na Mwana-Kondoo aliyekuwa amechinjwa, tangu kuwekwa misingi ya dunia; Yeye alistahili kuja na kukichukua kile Kitabu kutoka kwenye mkono wa kuume wa Yeye aketiye juu ya Kiti cha Enzi, na kukifungua hicho Kitabu, na kuzifungua Muhuri zake." Basi huyo Mwana-Kondoo, bila shaka, alikuwa

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Na sasa iwapo Ndiye pekee anayestahili . . .

34 Yeye aliishi hapa wakati mmoja pamoja nasi, duniani, katika mfano wa Mtu. Mungu aliishi katika Mwanawe, Kristo Yesu, kama Mungu-Mtu.

35 Ndipo Yeye akarudi Utukufuni, akiacha Neno hili, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona, kwa maana Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Utu wa Roho Mtakatifu, Mungu, akirudi katika mfano wa Yeye . . . Yesu alisema, "Nilitoka kwa Mungu; narudi kwa Mungu." Yeye alitoka Umilele, akashuka chini katika wakati; akatoka nje ya wakati, akarudi katika Umilele.

36 Na ulimwengu haukumjua Yeye. "Alikuwako ulimwenguni, kwa Yeye ulimwengu ulipata kuweko, wala ulimwengu haukumtambua. Bali wote waliompokea Yeye, wao . . . aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu.

37 Basi, sasa, sasa Yesu Kristo yuko pamoja nasi, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, bali ninyi mtaniona." Sasa kutakuwako na ulimwengu ambao haumwoni Yeye, na kutakuwako na "yeye" ambaye huona. "Kwa maana Mimi . . . " "Mimi" ni kijina cha nafsi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Nanyi, mwamini, mtamwona moja kwa moja hata ukamilifu wa dahari.

38 Waebrania 13:8, ilisema, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Mwangalie Yeye katika nguvu Zake, Bwana Yesu yule yule, upendo ule ule, maajabu yale yale, ishara zile zile zilizomfuata Yeye, zikiendelea moja kwa moja. Yeye yuko katika ule Mwili wa siri sasa, Mwili wa wale waliofufuka, kutoka dhambini kuingia Uzimani. Yeye yu aishi ndani yao.

39 Mungu katika Utukufu Wake mkuu, Mungu akijidhili, akitoka kwenye ile Nguzo ya Moto, hakuna mtu angaliweza kumgusa, akashuka katika mfano wa mwili wa mwanadamu ambapo angeweza kugusa, bali Yeye alizaliwa na bikira. Ndipo, kule nje, akitoa uhai Wake apate kuangikwa, kumsafisha mtu mwenye dhambi, Naye angeweza kuishi moja kwa moja kati ya wanadamu. Ni upendo wa jinsi gani Mungu alio nao kwa mwanadamu, hata angeweza alijifunua Mwenyewe, kufanya njia iliyo safi ili Yeye apate kuishi na kupenda miongoni mwa wanaume na wanawake. Ni zuri. Naam. Huyo ndiye Baba yetu.

40 Na tuzungumze Naye sasa hivi, Mwandishi wa kile Kitabu, kabla hatujazifungua kurasa.

41 Baba wetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunakuja Kwako, usiku wa leo, katika njia ambayo tuliahidiwa sisi, "Mkiniomba Mimi lo lote katika Jina Langu, hilo nitalifanya." Kwa hiyo hatuna haki, hatuna kitu tunachoweza kutoa, ila tu tunakuja

katika Jina la Bwana Yesu, tukijua ya kwamba uliahidi kusikia kupitia katika Jina hili.

42 Tena tunakuomba Wewe, tukijua ya kwamba tuna hapa, tunalofikiria usiku wa leo, moja ya masomo yaliyo muhimu sana ya siku hizi, *Muhuri Ya Mungu*. Baba, tunaomba, Bwana, tukijua ya kwamba kundi hili dogo la watu waliokusanyika hapa, kama nikiwakosesha, nitatoa hesabu kwa ajili yake kwenye ile Siku ya Hukumu. Na jana jioni, juu ya, *Alama Ya Mnyama*. Ee Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utuongoze na kuyaelekeza Maneno hayo. Jalia lisirudi bure, bali na litimize kile lililchokudusiwa wakati lilipoandikwa katika kile Kitabu.

43 Basi sasa njoo, Uliye Mtakatifu, chukua Neno la Mungu moja kwa moja kutoka kwenye Biblia, linene kupitia midomo ya binadamu, kuingia katika maskio ya binadamu, na utahiri kule kuzungumza na kusikia pia, ili kwamba tupate kutimiza kitu kwa njia ya kusanyiko hili, usiku wa leo; tukijua ya kwamba huenda kukawa na wengine hapa, kama ulimwengu ukidumu mwaka mwingine, hawatakuwa binadamu duniani.

44 Basi sasa tumo katika nyumba ya masahihisho, kwenye nyumba ya Mungu, ambapo tunapaswa kusimama kwa ajili ya kusahihiswa. Naomba kwamba Roho Mtakatifu anisahihishe mimi, na akifunge kinywa changu, kama ulivyofanya kinywa cha wale simba, pamoja na Danieli. Nawe unajua moyo wangu, kama neno moja ningezungumza kinyume ama kwa nafsi yangu. Naomba Roho Mtakatifu apake mafuta kila Neno. Nisimame tu kama chombo kitupu; Naye na aseme Neno la Mungu, usiku huu, kwa maana mioyo yetu iliyo na njaa inatamani kusikia kutoka Kwake. Tena jalia Yeye, aliyeiandika Biblia, aje na kuifasiri kwa watumishi Wako wanyenyekevu hapa. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

45 Sasa kwa ajili ya msingi mdogo tu, kuanza usiku wa leo, na, *Muhuri Ya Mungu*.

46 Msisahau, kesho usiku, tunawataka muwe na swali lenu. Na liandike vizuri, kisha uliweke jukwaani, mapema, ama mimbarani, mapema uwezavyo. Sasa somo hili kubwa tulilokuwa nalo jana usiku . . .

47 Usiku wa kwanza, wa juzijuzi, ilikuwa ni Kanisa na wakati wa kanisa, jinsi tulivyomwona Yesu akisimama katikati ya Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu, alionekana kama jiwe la yaspi na akiki, mwanzo na mwisho, Rubeni na Benyamini. Mnaona vile vinara vya taa saba, au miango ya taa imesimama, na upinde wa mvua juu yake, kama agano, na jinsi alivyoonekana. Na Sauti Yake ilikuwa sauti ya maji mengi, Kristo na Kanisa pia, wakizungumza pamoja; amefunga mshipi wa dhahabu karibu na sehemu ya matitini ya Kanisa, akafunika, akishikilia, Injili akishikilia haki ya Kristo juu ya Kanisa. Akisimama katika msingi wa shaba, hukumu ya Kiungu;

Mungu alimwaga hukumu Yake ya Kiungu juu ya Kristo, Naye akateseka, asiye na hatia kwa wenye hatia.

48 Halafu, kuona jinsi ilivyoanza na kanisa la Waefeso; halafu wakati wa pili wa kanisa; wakati wa tatu wa kanisa; wakati wa nne wa kanisa, ile miaka elfu moja mia tano ya nyakati za giza na kupitia kwenye Wakati wa Kiluteri; na Wakati wa Filadelfia; na kuingia katika Wakati wa Laodikia, ule wakati wa mwisho.

49 Kuona katika Agano la Kale, jinsi walivyoonyeshwa vizuri kwa mfano hapo mwanzo, katika Suleimani, kote kote kupitia kwenye wakati wa Ahabu, ule wakati wa giza. Ndipo tukaona, kama Yezebeli, Ahabu, mhubiri wa mpakani, ama mtu asiye thabiti. Ni kama tu wengi wa wafuasi wa kanisa walio na uvuguvugu leo, watu, wasio thabiti; kanisani leo, kesho unaweza kuwatarajia mahali po pote; wakipatana, wakiachilia, wakiambatana na ulimwengu, hata hivyo wakijiita Wakristo. Naye Ahabu, kaktika hali hiyo, alimpenda maskini mwanamke mrembo, ingawa mwovu kama wote akaenda. Ndipo akafanya ndoa naye, ndipo akaleta ibada za sanamu katika Israeli, moja kwa moja katika wakati wenye giza sana wa Israeli, wakati wa giza. Naam, tunaona ya kwamba walikuwa wametoka kule wakiwa na msimamo wa hali ya juu, kisha wakatoka, na hatimaye wakawa na uvuguvugu, wakashuka mpaka Mungu akawatema kutoka katika kinywa Chake na akawakubali Mataifa.

50 Na sasa tunaona kwamba wao walikuwa wameanza na wa kwanza, Ka—Kanisa la Efeso, hapo mwanzo, katika wakati wa kanisa; wakati wa pili wa kanisa ukaanza kuwa baridi na kuwa na uvuguvugu; ukaingia moja kwa moja ndani, halafu wakati wa giza. Na kama tu—kama siku ile, Ahabu akioa mwabudu sanamu, Yezebeli, kisha akaleta kuabudu sanamu katika Israeli; ndipo Uprotestanti ukaoa Urumi, Ukatoliki, na kuleta ibada za sanamu kanisani. Wakatoka kupitia Martin Luther; moja kwa moja kupitia John Wesley; mpaka wakaingia kwenye Pentekoste; kisha wakatoka, hata wakatapikwa kutoka katika kinywa cha Mungu. Ndipo Mungu atairudisha kwa Myahudi tena, kamilifu tu.

51 Naam, najua mimi. . .Mnasema, sasa, mimi ni mwenye kuonyesha kwa mifano. Hiyo ni kweli. Maana, najua, ninajua jambo moja, kama ninaelekea kwenye kivuli changu nami nione vile kivuli changu kilivyo, nina wazo la vile mimi nilivyo; au mimi ni mnyama mwenye miguu minne, ama ndege mwenye mabawa, ama cho chote kile, kitaonyeshwa kwenye kivuli.

52 Nalo Agano la Kale lilikuwa kivuli cha lile Jipya. Tulipata jambo hilo jana usiku, katika Ufunuo 12, yule mwanamke mwenye torati chini ya miguu yake, mwezi na jua kichwani mwake, na mfano. Jinsi, vitu hivyo vyote, Waebrania sura ya 11 inatwambia, wote walikuwa mifano na vivuli. Ninaamini,

Waebrania 12, ilisema yeye, "Kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, tupate kupiga mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu." Naam, tumeona mambo hayo. Halafu jana jioni . . .

53 Tulichukua nyuma hapa, kupata kujua, ama—ama, juzi usiku. Tunaona basi, kwamba, kanisa la kwanza, jinsi lilivyoanza. Lilizinduliwa na kuanzishwa kwenye siku ya Pentekoste, ambapo Roho Mtakatifu alimwagwa juu ya waamini. Nasi tuliona walivyotenda hawa waamini, na jinsi Yeye alivyotenda juu yao, na yale waliyofanya, na ishara na maajabu yaliyowafuata.

54 Kisha tunaona, katika kumalizia kwa wakati huo wa kanisa, yapata miaka mia tatu, wao walianzisha uvumi kati yao, ulioitwa, "fundisho la—la Nikolai." Kisha tunaona, lilikuwa "matendo," kwanza.

Katika wakati wa kanisa uliofuata, likawa "fundisho."

Kisha likawa "mateso," katika wakati wa giza.

55 Halafu tukaja upande ule mwingine, upande huu, tukaona kwamba lilianguliwa moja kwa moja pamoja na makanisa ya Kiprotestanti yaliyotoka.

56 Kisha tunarudi nyuma tena basi na kuona jinsi uvuguvugu wote uko hapa katika mwisho wa ule wakati, upande *huu*, jinsi wote unavyoingia baridi. Kama tu ulivyofanya chini ya Wayahudi, ndivyo unavyofanya chini ya Mataifa; ukipata baridi unapoelekea upande *huu*, kivuli, kikififia.

57 Kama tu ilivyokuwa, katika siku za Wesley, nasi tulileta jambo hilo usiku wa jana, na Luther. Jinsi mlivyokuwa na ufufuo mkuu, lakini, zamu ya pili, ukaanza kupata baridi. Zamu iliyofuata, ukapata baridi zaidi. Na sasa ni kundi tu la kanuni za imani na taratibu. Ni hayo tu. Mnaona? Na hivyo ndiyo imekuwa kila mahali. Kwa hiyo tumefundisha hayo.

58 Naam, kufunga sasa, sikilizeni, ili kwamba mwe na hakika mtakumbuka. Mimi siwahukumu Wakatoliki, wala siwahukumu Waprotestanti, kwa maana kutoka kwa wote wawili na hao wote unatoka Uzao wa Mungu, kwa kuteuliwa. Hao waliochaguliwa kwa ajili ya Uzima wataliona Hilo na kutembea ndani Yake. Hao ambao hawawezi kuona, wanatembea gizani. Hilo ni juu ya Mungu. Mungu hufanya jambo hilo. Yeye aliapa na akamwahidi Ibrahimu angemwokoa pamoja na Mzao wake. Naam, kama una Mzao wa Ibrahimu, una Uzima wa Milele, hivyo tu, nawe ni mrithi kulingana na ahadi. Na yote ni kwa neema na kwa kuteuliwa na Mungu.

59 Sasa angalia, katika hili hapa. Nami tu wakati mwingine . . . labda kama nilihubiri zaidi, ama kufundisha zaidi. Imekuwa miaka kadha. Huu ndio mkutano wa kwanza wa kufundisha

nimekuwa nao, kwa yapata miaka minane. Na ni kidogo tu, labda kumeingia kutu, mahali mahali. Wakati wo wote mnapo—mnapo-. . . Niulizeni swali lo lote mnalotaka; liwekeni jukwaani, ama mimbarani, nami nitafurahia kulipata.

60 Sasa angalia. Lakini nijuavyo mimi juu Yake, sikufundishwa Hilo na mwanadamu, na seminari. Niliomba mpaka nikapata ufunuo wake, nao ulipaswa kulingana na Neno la Mungu.

61 Katika Agano la Kale, wao walikuwa na njia tatu za kujua ujumbe. Njia ya kwanza wangepata kujua, ilikuwa aidha imeandikwa katika torati; jambo la pili lilikuwa nabii; ama jambo la pili lilikuwa Urimu na Thumimu. Sasa mwalimu ye yote anajua Urimu na Thumimu ilikuwa ni kitu gani. Ilikuwa ni—ni nuru iliyomulika kwenye kifuniko cha kifuani cha Haruni, walichoning'iniza hekaluni. Naam, kama nabii alitabiri, na hiyo Nuru haikumulika kwenye Urimu na Thumimu, ilikuwa ni makosa. Hiyo ilikuwa ni jibu la Kiungu la Mungu, "Ilikuwa ni makosa." Halafu kama wao. . . Kama mwotaji aliota ndoto, na haikumulika kwenye Urimu na Thumimu, ilikuwa ni makosa.

62 Naam, ile Urimu na Thumimu imeondolewa, kwa hali hiyo, bali *Hii* ndiyo Urimu na Thumimu ya Mungu sasa, Biblia. Kama nabii, ama mwotaji, ama cho chote kile, ama mwalimu, hajaweka msingi wa nadharia yake kwenye BWANA ASEMA HIVI, siiamini, mnaona. Haina budi kuja papa *Hapa*, kutoka Mwanzo hata Ufunuo, si katika mahali pamoja tu. Haina budi kupitia kwenye Biblia na kuifunganisha pamoja hasa. Naam, bwana. Haina budi kuambatana na lingine lote, na kushikamana yote pamoja. Kama hufanyi hivyo, ungechukua jambo moja na kusema ya kwamba hiyo ni pagatorio, kisha uhubiri Ukatoliki kutoka kwenye Biblia. Bali halina budi kuambatana kabisa kutoka Mwanzo hata Ufunuo, kufanya picha dhahiri. Hiyo ni kweli.

63 Na Roho Mtakatifu ndiye anayeisafisha picha Hii kwa ajili yako, kama tu utamruhusu kufanya jambo hilo. Yeye atakuongoza katika Nuru yote. Biblia ilisema jambo hilo. Yesu alisema Yeye angefanya jambo hilo.

64 Sasa angalia tu-. . . Tena, sasa, tunaona kile walichofanya kule. Halafu, baada ya kitambo kidogo, wao wakapata fundisho. Wakapata mateso. Wakatoka.

65 Halafu tunakuja kuona, ya kwamba katika siku hii sasa, kwamba Biblia ilitabiri ya kwamba kungekuwa na wakati ambapo watu wangepokea alama fulani, na alama ya mnyama.

66 Kila wakati kitu fulani kidogo kinapozuka nchini, kila mtu alisema, "Hiyo ni alama ya mnyama." Wakati wale wa kale. . . Nilikuwa tu nimefanywa kasisi katika kanisa la Kibatisti, wakati niliposikia juu ya N.R.A. Vema, kila mtu alisema, "Hiyo ndiyo ile alama ya mnyama." Halafu basi kila kitu kinaanza moja kwa moja, "Ni alama ya mnyama."

67 Na sasa wao wanasema, “Hii hapa Urusi inashuka, ukomunisti, ndiyo alama ya mnyama.” Lakini, ni uongo. Hiyo siyo alama ya mnyama. Biblia inatwambia alama ya mnyama ni nini. Alama ya mnyama si kupinga dini na kupinga nchi kukuu kunaoinuka namna hiyo. Ukomunisti si Urusi; ukomunisti ni roho. Yote ni . . . Haitu—haitupasi kufadhaika juu ya Urusi.

68 Kuoza kwetu wenyewe ndiko kunakotuua. Ukomunisti unaingia moja kwa moja miongoni mwa makanisa yetu na kila kitu kingine, mwajua jambo hilo, na katika mashule yetu, katika majumba yetu, kila mahali, katika taifa letu. Kitu hicho chote kimeliwa na mabuu. Ndege anayepekua tofaa hailidhuru; ni yule buu aliye kwenye sehemu ya katikati anayeliharibu tofaa. Hivyo ndiyo ilivyo, ni kule kuoza miongoni mwetu. Kwenda, kujiita wenyewe Wakristo, na kutenda kama ulimwengu, kuvalia kama ulimwengu, na kushiriki ya ulimwengu, na kujiita wenyewe . . . Ulimwengu ni mgonjwa na umechoshwa na mambo kama hayo. Wala si ulimwengu tu, Wakristo wengi wamechoshwa, pia. Naam.

69 Mara nyingi nimesema, “Mungu na asaidie siku ambayo watu watakuwa vile wanavyopaswa kuwa. Kama nilikuwa ninampinga Yeye, ningesema nilikuwa ninampinga Yeye, ningempinga Yeye katika kila kitu ambacho ningekuwa.” Bali mimi ninamuunga mkono, ninampenda, pia ninamwamini Yeye. Na—na maisha yangu yomo mikononi Mwake, kufanya analotaka kufanya, kwa maana ninaamini ya kwamba Ukristo ndio Kweli. Hiyo ni kweli. Ninaamini ni Kweli.

70 Katika kutembea ulimwenguni, na kuangalia katika itikadi mbalimbali, na kadhalika, waanzilishi wake wote wamekufa na wamelala kabarini, nao wana theolojia. Huo ndio umbali tu ambao kanisa la Kikristo linaenda na jambo hilo, hata hivyo.

71 “Bali hao wamjuao Mungu wao watatenda mambo makuu.” Na Nguvu za Yesu Kristo aliyefufuka zinaishi katika mwanadamu. [Ndugu Branham anagongagonga mimbara mara sita—Mh.] Hiyo ni kweli. Yeye hajakufa; amefufuka. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, na mambo nifanyayo nanyi pia mtayafanya.” Naam, bwana.

72 Ndipo ulimwengu unapoangalia nje na kusema, “Ushupavu wa dini.” Mnaona ambapo tulilichukua jana usiku, kwa msaada wa Mungu.

73 Naam, tunaona ya kwamba kitu cha kwanza kilichopata kuinuka kufanya mfano wo wote wa mnyama, kwa vyo vyote, ama . . . *Mnyama* maana yake ni “nguvu.” Tulipitia katika mifano yote na kila kitu, jana usiku, kuthibitisha ya kwamba mnyama alikuwa ni nguvu. Naye hakutoka Urusi. Alitoka Rumi. Hiyo ni kweli. Alitoka Rumi.

74 Na haikuwa—haikuwa kundi la watu. Haikuwa utaratibu wa kisiasa. Ilikuwa ni shirika la kidini. Ilikuwa ni kanisa “linalokaa

juu ya vilima saba," likiwa na mtu mmoja aliyekuwa na mamlaka ya kutawala kila mahali ulimwenguni, mle ndani. Kweli kabisa. Nasi tunaona ya kwamba ilikuwa ni mwanamke, na kumwonyesha dhahiri tu. Si kuchukua fasiri yangu mwenyewe; kusoma tu Bibliani. Ya kwamba, hakuna mahali pengine ulimwenguni, hakuna mji mwingine ulimwenguni, unaotawala dunia nzima. Katika kila taifa, mlia huo wa Urumi unatokeza kama katika vile vidole kumi vya lile ono la Danieli, nasi tunaona ya kwamba huo ulikuwa ni Mji wa Vatican.

75 Haikosi Wakatoliki dazani moja waaminifu waliokuwa wameketi hapa jana usiku. Wao waliketi kwa utulivu na kusikiliza. Wao ni waaminifu. Wana njaa.

76 Naam, hauwezi kubishana na kasisi. Yeye hatabishana, maana, kasisi, "Kama kanisa likisema lo lote mbali na Biblia hii, kanisa ni kweli." Kwangu mimi, Biblia ni kweli na kanisa limekosea. Mnoana? Hauwezi kubishana nao. Wao, huna budi . . . Hakuna njia ya kubishana. Hakuna njia ya kubishana. Hakuna njia ya kuhojiana wala kubishana. Kwa maana, wao wanaamini, "Kile kanisa lisemacho, basi! Ndicho hicho, kile lisemacho kanisa, haidhuru Biblia inasema nini. Ni kile lisemacho kanisa!" Wao wanaamini kanisa. Tunaamini Biblia.

77 Sasa tunaona kwamba yeye aliitwa . . . Kanisa lilikuwa ni mwanamke. Nalo liliitwa neno baya, na chafu la "KAHABA," halafu lilikuwa "MAMA WA MAKAHABA." Nasi tunaona ya kwamba kanisa Katoliki lilikuwa kanisa mama la kwanza. Lilikuwa kile hasa lilichosema lilikuwa. Ndilo kanisa la kwanza kuunda madhehebu. Ni lini Mungu alipowahi kuunda madhehebu, ilikuwa ni kanisa Katoliki. Madhehebu ya kwanza yaliyopata kuundwa ulimwengini, ya dini ya Kikristo, kanisa Katoliki. Sasa . . .

78 Halafu, hatimaye, lilikuwa "MAMA WA MAKAHABA." Liliyazaa makanisa, yaliyofanana nalo, maana wasingeweza kuwa ni wavulana. Iliyabidi yawe ni wasichana, nasi tunaona ya kwamba kanisa la Kiprotestanti lilitokana na kanisa Katoliki. Kwa kuyachunguza Maandiko, na kuangalia kwenye kitabu chako cha historia, tunaona ya kwamba kanisa la Kiprotestanti ndilo matokeo yake. Naye Mprotestanti asingeweza kumkemea Mkatoliki, kwa maana, wote wawili, linasema wao walikuwa "MAKAHABA" na "KAHABA." Huo ni ufidhuli, lakini hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli.

79 Angalia, ndipo, yeye alisema, "Na," katika Marekani, wao walisema, "na tufanye sanamu ya mnyama." Kama yule mnyama alikuwa ni nguvu, na hizo nguvu zilikuwa ni madhehebu; si kuchukua nadharia sasa. Hilo ni Neno la Mungu. Madhehebu ya kanisa Katoliki yalijiandaa pamoja yakaunda madhe- . . . kukubali. Nao wakaweka, wanachoita, wale "mapadre wa mwanzoni" pamoja, nao wakaliunda kanisa

Katoliki madhehebu, na kufanya u—u—u—utaratibu wa dini, na yale waliyoamini na yale wangefundisha, imani ya watu wote. Nao wakaishurutisha kwa watu, kwa adhabu.

80 Ndipo wakati Martin Luther alipotoka, akiona Roho wa Mungu akimwongoza atoke. Badala ya kuwaacha watu wakae huru, yeye alilifanya kanisa madhehebu; sanamu iliyofanana na yule mnyama, nguvu za kisiasa zilizolinganishwa nalo. Badala ya kuwaacha watu watembee jinsi Mungu alivyowapa nuru, wao waliunda madhehebu chini ya utaratibu, nao hawana budi kudumisha utaratibu huo.

81 Mungu alitoka moja kwa moja akaingia katika kanisa la Kimethodisti. Methodisti ilikuwa na ufufuo ulioenea duniani kote; Roho Mtakatifu akiwa pamoja nao, akifundisha utakaso. Na muda si muda, walipofanya jambo hilo, ndipo wakalifanya kanisa madhehebu, wakafanya sanamu ya mnyama, hiyo ni kweli, nguvu za kisiasa, za kimadhehebu, kuwafungamanisha watu wa Mungu kwa kanuni za imani; badala ya kuwa huru kuabudu na kutembea katika nuru wakati nuru ilipoangazwa njiani mwao.

82 Waliwarudisha nyuma, katika wakati huo. Hiyo ilikuwa nuru nzuri kwa ajili ya mahali hapo. Hiyo ilikuwa ndiyo nuru kwa ajili ya—kwa ajili ya kanisa la Pergamo.

83 Na kanisa la Filadelfia je? Hiyo ni nuru nyingine. Lakini, mnaona, haidhuru walifanya madhehebu namna gani, Mungu aliondoka moja kwa moja kutoka kwenye wakati *huu* wa kanisa, haidhuru, akamtuma mtu, jina lake John Wesley. Luther asingeweza kuifuata, maana hakuiamini. Alikuwa tayari ameunda madhehebu *huko* nyuma.

84 Ndipo John Wesley akaunda madhehebu kwelikweli, hata akafikia mahali fulani. Ilikuwa ni saa ya wakati *huu* wa kanisa kuingia. Mungu akatuma kundi la Kipentekoste; likatoka likaenda hapa nje na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Loo, Methodisti ikasema, "A-ha. Ahaa! Hatuwezi kuambatana na jambo Hilo. A-ha! Hatuamini katika upuzi huo. Lo, la." Mbona? *Hii* ndiyo nuru waliyokuwa wakitembealea, *hapa*; hii *hapa* nuru ya upande *huu* sasa.

85 Tunashika njia tukielekea kwenye machweo ya jua. Mnakumbuka aliyosema nabii? "Itakuwa siku itakayokuwa na mawingu, si usiku wala mchana, lakini wakati wa jioni kutakuwako Nuru." Ile Nuru ambayo wakati mmoja iliangaza katika nchi ya mashariki kwa ajili ya Wayahudi, katika mashariki (Wayahudi ni watu wa mashariki), inawaangazia Mataifa; Nuru ile ile, Roho Mtakatifu yule yule, katika siku za mwisho upande huu, ubatizo ule ule wa Roho. Tumepitia katika nyakati hizi zote kupitia hapa, ambapo hamna wakati wa Nuru wala wakati wa giza, bali ni siku yenye mawingu,

na utusitusi; bali papa *hapa*, kama nuru ilivyoangaza jinsi tu ilivyofanya pale.

86 Hiyo ndiyo sababu, "Alionekana kama jiwe la yaspi na akiki; Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho; Yeye Aliyekuwako, Ambaye Yuko, na Atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi; Nyota ya Asubuhi." Hilo hapo. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Natumaini mnaliona.

87 Basi, kumbuka, ya kwamba tuliona, bila kosa moja, ya kwamba alama ya mnyama ni alama ya ukengeufu, hiyo ni kusema, wafuasi wa kanisa wakishikilia kanisa lao badala ya kutembea katika Nuru. Wao waliikataa Nuru, na hakuna kilichosalia ila giza. Hiyo ni kweli, kwa Katoliki na Protestanti pia. Kuna "mnyama, na kahaba," naye ana binti "makahaba." Na hawa binti makahaba, walipotoka, walikuwa bikira kutokana na Nuru ya wakati huo, nao wakaunda madhehebu na kuwaleta watu hapa chini, kuwarudisha humu ndani, akiwafanya kitu cha namna ile ile ambacho Rumi ilikuwa hapo mwanzo. Biblia ilisema jambo hilo. "Yule mnyama; na sanamu ya mnyama; herufi za jina lake," na kadhalika.

88 Jinsi tulivyopitia kwenye jambo hilo lote, jana usiku, nayo Biblia kwa udhahiri. . .si nadharia ya mtu fulani. Bali Biblia ilieleza jambo hilo, ya kwamba yule mnyama mwenye vichwa saba na pembe kumi alitoka [Yawezekana pawe ni mahali patupu kwenye kanda—Mh.] kutoka Rumi, alikuwa kule katika Rumi, na alikuwa, "Yeye aliyekuwako, ambaye hayuko; na ambaye yuko, na ambaye hayuko," papa mmoja baada ya mwingine, papa mmoja baada ya mwingine, na wataenda kwenye uharibifu. Nasi tukaona kwamba mwanamke yuyo huyo mzee alizaa wasichana fulani. Walikuwa mabikira tangu mwanzo, wakatembea katika Nuru waliyokuwa nayo. Kisha wakaanza kutenda kama makahaba, nao wakarudi kufanya jambo lile lile mama yao afanyalo. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara mbili.] Hakika. Hakika.

89 Hebu niwaambie jambo fulani, enyi wanawake. Sikilizeni. Huenda msiwe na matumaini mengi sana kwangu sasa, wakati ninapokemea mambo haya. Na si kuwaudhi; ni kuwasaidia. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Lakini mnapoona watu, makanisa leo, yakiwaruhusu wanawake wao. . .Naam, ni—nitawafikia wanaume, pia. Lakini kuwaruhusu wanawake wao kufanya jinsi wanavyofanya leo, nao wakikiri Ukristo! Siwalaumu ninyi wanawake; nitawalaumu, baada ya usiku wa leo. Lakini, angalieni, si—siwalaumu ninyi wanawake sasa. Lakini, dada yangu, wengi wa hawa waalimu wa seminari huku, ama waalimu wa makaburini, ama cho chote mnachoiita, kutoka mahali fulani hapa, wanawaruhusu tu kutembea katika udanganyifu huo. Biblia ilisema, "Wao walikuwa vipofu, wakiongoza vipofu." Ni kweli. Sasa . . .

90 Pia, Yesu, akiona jambo hili, na akijua ya kwamba baadhi ya hayo makanisa ya Kiprotestanti yangetembea moja kwa moja kwenye lango la Nuru, na kugeuka. Yesu, katika Mathayo 24:24, alisema ya kwamba ingekuwa namna hiyo, "Mpinga Kristo angefanana sana na aliye wa kweli, hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini."

91 Naam, mnaona, Urumi, Ukatoliki, loo, umewagonga baadhi yenu Waprotestanti kichwani. Lakini, mtu aliye na neema kidogo, ninino kidogo...anayejua machache juu ya Biblia, yeye ataacha na kuondoka. Hiyo ni kweli. Ushawishi wake ni mweusi kwake; yeye anajua hakuna kitu kwake, upuzi huo wote wanaofundisha. Hamna Maandiko kwa ajili ya jambo hilo; mara kwa mara, wanayagusia kidogo.

92 Uongo mkubwa sana uliopata kusemwa, ulikuwa na Kweli nyingi sana kwake. Hiyo ni kweli. Na wa kwanza, Shetani akizungumza na Hawa, alisema Kweli nyingi sana. Bali alikuwa na kama, chini yake, alikuwa na uongo ambao ulimhukumu, na kuangamiza kizazi chote, viumbe wote. Hiyo ni kweli.

93 Unapaswa kuangalia jambo hilo. Halina budi kuja Kweli *hapa* na Kweli *hapa*, Kweli *hapa* na Kweli *pale*. Kila sehemu yake, ni Kweli; likifuatana vile vile, kote kote.

94 Halafu tena jinsi watu wanavyoweza kuona kanisa la mwanzoni kule nyuma liliangazwa na kinara cha mshumaa halafu upande *huu* kuona jambo lile lile likitukia ambalo lilitukia kule nyuma, na Neno la Mungu likisema ingekuwa ni "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele." Na kulikataa? Inaonyesha wao wameikataa Nuru, na wanatembea gizani; jambo pekee lililosalia.

95 Ni kweli, ndugu yangu. Sisemi jambo hilo kuwa mwerevu. Mungu anajua hilo. Yeye anaujua moyo wangu. Nina huduma, na mengi mbele yangu bado. Nami nikijua ya kwamba siku moja, kwenye Kiti cha Hukumu, nitawajibika kwa mambo haya. Hiyo ni kweli kabisa. Ningepatwa kuwa mshtaki wa uongo, mwalimu wa uongo, halafu Mungu angenihukumu. Hiyo ni kweli. Bali kama najua Kweli ya mambo haya, nami siwaambii, Yeye atanihukumu basi, hakika.

96 Kamwambia mlinzi, "Angalia! Kama ukikosa kuonya, basi nita—nitataka kutoka mkono wako. Lakini kama ukionya, nao wanaendelea, watakufa katika dhambi yao, bali sitaitaka kutoka mkono wako. Utakuwa huru."

97 Kwa hiyo tunataka kuwa waangalifu kwamba tunajua Kweli ni nini, kulingana na Biblia. Na jinsi wakati huo ulivyoanza, na jinsi walivyofanya, na leo kuona kanisa la Kiprotestanti moja kwa moja chini hasa.

98 Angalia hapa. Ilikuwa kwamba, wakati mrefu uliopita, nanyi watu wa utakatifu, ilikuwa ni makosa kwenu wanawake kukata nywele zenu. Ubaya wake na uzuri wake ulikuwa ni nini? Wakati

Biblia iliposema ya kwamba, “Mwanamke ye yote akikata nywele zake, mumewe ana haki ya kumpa talaka.” Mafundisho dhahiri, lakini hiyo ni Biblia.

99 Nanyi wanawake, mnatoka hapa nje na kukata nyasi uani mwenu, mmevaa ovaroli, na mkiwa na mavazi ya mwanamume. Nayo Biblia ilisema, Mwenyezi Mungu alisema, “Mwanamke atakayevaa vazi limpasalo mwanamume, ni chukizo, uchafu mbele za Mungu.” Nanyi mnafanya jambo hilo.

100 Nanyi mnavuta sigara, mnaenda kwenye dansi na sinema, na mngali ni wafuasi wa kanisa. Mnaonyesha mmechukua kitu fulani; hamjaandikwa Mbinguni, Roho Mtakatifu. Baada ya kitambo kidogo tutaingilia jambo hilo, na kuwaonyesha vinginevyo. Naam, hilo ni jambo ndogo tu.

101 Nanyi wanaume, mnaenda kanisani, mkitembea barabarani mkiwa na msokoto mdomoni mwenu, kama ma—maksai wa Texas, aliyeng’olewa pembe. Kisha mnapata . . . Sisemi jambo hilo kwa mzaha. Siamini katika kufanya mzaha mimbarani. Ninasema jambo hilo ni Kweli. Wanashuka kwenda barabarani, nao wataketi katika mahali, na kudanganya, na kuiba, na kudanganyana wao kwa wao, nao ni mashemasi kwenye halmashauri ya kanisa.

102 Wanashuka kwenda makanisani na kucheza hizi karata za kale, hiyo si kitu ulimwenguni ila bahati nasibu ya kawaida, iliyo duni. Hiyo ni kweli. Nanyi mnafanya jambo hilo, kisha mnapiga makelele juu ya bahati nasibu ya farasi. Ninyi ni wabaya vivyo hivyo, katika makanisa yenu, enyi Wamethodisti, Wabatisti, na Wapentekoste, ye yote yule anayefanya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Nanyi mnajua hiyo ni kweli. Bali ni nini? Mnarundikana moja kwa moja kama mama yenu kule nyuma. Jambo lile lile hasa, na nyungu haiwezi kuiita birika kwamba ni nyeusi. Basi kuna roho hiyo ya mambo.

103 Lakini mimi sina neno dhidi ya Wakatoliki. Sina kitu dhidi ya Wamethodisti, wala Wabatisti, wala Wapresbiteri. Mungu anao watu, Wazao wa Ibrahimu, kule nje. Sina kitu dhidi ya hao watu. Ni kuhusu makanisa yao, yaliyojiundia madhehebu pale, nao wanaliabudu kanisa badala ya Mungu. Loo, ninyi Waprotestanti hamtaki kuamini jambo hilo, bali mnafanya jambo hilo, hata hivyo. Nitasema, je! wewe ni Mkristo?

104 Vema, hapa si muda mrefu uliopita, Ndugu Bosworth alimuuliza msichana fulani, kasema, “Je! wewe ni Mkristo?”

105 Akasema, “Ati Mkristo? Nataka ujue, ninawasha mshumaa kila usiku!”

106 Vema, sasa enyi Waprotestanti mnafikiri hilo ni kitu? Je! wewe ni Mkristo? “Nataka ujue, mimi ni Methodisti,” ama “Mbatisti.” Vema, hilo halimaanishi kitu ila umetoka nje ya siku ya neema, kwa nafsi yako, kwangu mimi; hiyo ni kweli, kama hivyo ndivyo tu wewe ulivyo, Mmethodisti tu, ama Mbatisti.

Kama wewe si Mkristo katika hiyo Methodisti, ama Batisti, ama kanisa Katoliki, umepotea. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hiyo ndiyo alama yako hasa.

107 Alama zote mbili ni za kiroho. Sasa nitawathibitishia kwa Biblia. Alama hizo zote mbili ni alama za kiroho.

108 Watu wengi walifikiri, "Wao watazunguka na kuchanja kitu fulani katika kipaji cha uso wako, na kuchanja kitu fulani katika mkono wako." Tuliona, usiku wa jana, kwamba hiyo ilikuwa ni uongo. Naam, Bwana. Hilo ni kosa. Ni alama ya kiroho. Ime—imefichwa sana. Basi, angalia, mara nyingi . . .

109 Sasa najua jambo hili huenda linatimua manyoya mengi, na li—li—linaonekana ligumu. Bali lita—litanyoka kama tukininino tu. . .na kumpa Mungu nafasi ndogo. Si—simaanishi kuwa mjeuri, lakini ni—ninajaribu tu kusema kweli, kwa moyo wangu wote.

110 Wakati Yesu alipoona kanisa hilo la Kiprotestanti limeanguka kutoka kwenye kanisa hilo la Katoliki kule ng'ambo, likatoka na kurudi moja kwa moja, na kurudi tena jinsi tu walivyofanya, Yeye alisema, "Ile roho itafanana sana, hata ingewapoteza walio wateule . . . "

111 Mlitambua, enyi marafiki Wakristo, ya kwamba mpinga Kristo, alama ya mnyama ni gani? Yule mpinga Kristo, mtu ye yote anajua ya kwamba yule mpinga Kristo pale, hiyo ndiyo alama yake, ni. . .ya nguvu zake. Na, mnaona, ni mnyama, ni nguvu. Kuna nguvu za kanisa Katoliki. Kuna nguvu za kanisa la Kimethodisti.

112 Nilienda, hapa si muda mrefu uliopita, kwa muungwana mzuri sana. Kama sijakosea, yeye anaketi moja kwa moja hapa kanisani usiku huu. Na maskini Edith Wright na hao wengine wakaja mkutanoni moja kwa moja hapa, si maili ishirini kutoka mahali hapa. Basi, sisi, hao watu. . .Nilikuwa tu ninahubiri Injili ya wokovu. Ilimbidi kupanda juu ya motokaa kufika mahali pale. Basi usiku huo, mchungaji akaniita moja kwa moja, kasema, "Ninasikitika kukwambia, Kasisi Branham. Lakini wao waliniambia walikuwa na wagonjwa fulani walioingia mle ndani, na mtu wetu wa jimbo akaja na kusema, 'Hakuna kuponya Kiungu katika kanisa la Methodisti.' Kwa hiyo itakubidi kwenda jukwaani, uombe ruhusa ya kuondoka, na uliache kusanyiko." Hiyo ni kweli.

113 Kwa nini? Nguvu za kanisa la Methodisti. Hizo ni nguvu za yule mnyama. Kanisa la Kibatisti vivyo hivyo; Wakampbeli, na Mluteri, na wengine wote, na Wapentekoste, ni wabaya vile vile. Hiyo ni kweli. Nimekuwa na Wapentekoste. . .Na Waasemblies of God wameingia katika halmashauri ya makanisa, ambayo ni—ni. . .Wao walijiingiza moja kwa moja humu, wakiwa na yule "mama" kahaba wa kale. Kwa hiyo kila shirika la kanisa linatoka Rumi. Huko ndiko kwenye mama wa yote hayo. Nami

si mtakatifu wa Siku za Baadaye, wala Mvua ya Siku za Baadaye, ama cho chote kile mnacholiita. Sitaki . . . Mimi si mmoja wa hayo.

114 Lakini ninamaanisha jambo hili, ya kwamba wanaume na wanawake wanapaswa kuwa huru katika Kristo Yesu, kutembea katika Nuru. Na kila kanisa linapaswa kuwa jambo lile lile. Hiyo ni kweli.

115 Naam, angalia hili, jinsi Biblia . . . Pata jambo hilo. Madhehebu hayo, kumbukeni, hapo ndipo yalipo, papo hapo. Nasi tunaona, ya kwamba wakati kanisa Katoliki lilipoanza nyuma kule, walipata ubatizo wa uongo waliotoka noa, kunyunyizia maji badala ya kubatiza. Hakuna Maandiko katika Biblia kwa ajili ya jambo hilo. Na si jambo hilo tu, bali Roho Mtakatifu, na ubatizo wa maji, na taratibu, na vyeo, na cho chote kile, kudhihaki tu ulio wa kweli. Wala hakuna muhudumu nchini, ambaye anaweza kunionyesha mahali pamoja ambapo jambo hilo lilipata kufanywa katika kanisa la mwanzoni. Hiyo ni kweli. Haliko katika Biblia. Bali wao walitoka nalo, nasi tunalikubali moja kwa moja. Mnaona mahali ambapo tunarudi moja kwa moja?

116 Basi leo mnashangaa mbona hatuna ufufuo. Hivyo ndivyo ilivyo, ndugu. Tunachohitaji leo ni ufufuo mzuri wa mtindo wa kale, wa Mtakatifu Paulo, na Roho Mtakatifu wa Biblia arudi nchini tena. Hilo ndilo tunalohitaji. Sasa . . .

117 Nao wakachukua "alama ya mnyama," ama "sarufi ya jina lake," waliyemfanyia sanamu. Ile sanamu ilikuwa ni madhehebu kama tu kanisa Katoliki. Wao walilifanya madhehebu na kufanya sanamu ya kanisa Katoliki. Hivi kanisa la Kimethodisti ni sanamu yake; kanisa la Kibatisti, kanisa la Kipresbiteri, kanisa la Kipentekoste, kanisa la Utakatifu, Kanisa la Pilgrim Holiness, na la Muungano wa Ndugu? Kila moja lililounda madhehebu, lilitoa mfano wake kule. Halijapata kuwa katika Biblia ya Mungu. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara moja—Mh.] Hiyo ni kweli. Madhehebu; kufanya madhehebu!

118 Mungu ndiye kiongozi. Lirudishe jambo hilo nyuma kabisa utakavyo. Waangalie Israeli, wakipanda kutoka Misri.

119 Na hao Wamoabu wote wakisimama pale, wakiwa wa kimsingi, wakitoa sadaka; madhabahu saba, ninino saba . . . kondoo saba, zikinena juu ya kuja kwa Kristo; maksai saba, dhabihu iliyo safi. Papo hapo, nabii wake mashuhuri akisimama pale, Balaam, kuwalaani Israeli. Na hao hapo Israeli . . . Hao hapo Wamoabu, taifa kubwa. Kulikuweko na Waamori na kadhalika, taifa kubwa, limejiandaa pamoja kama taifa.

120 Nao Israeli walikuwa wametawanyika kule nje kondeni wakiwa na kundi la mahema. Wao walikuwa "wasafiri na wageni, wakiutafuta Mji ujao," baina ya madhehebu hasa. Nao walifanya nini? Walikuwa na ishara na maajabu yakiwafuata.

Hawa hawakuwa navyo; nao waliwaonea hao wivu. Hizo zilikuwa ni roho.

121 Mungu humchukua mtu Wake, bali si Roho Wake. Yeye alimchukua Eliya, ndipo roho yake ikamjia Elisha; miaka kadha baadaye, ikaja juu ya Yohana Mbatizaji; imebashiriwa tena katika siku ya mwisho.

122 Ibilisi anachukua mtu wake, bali si roho wake. Huyo mwalimu yule yule wa kidini aliyemhukumu Yesu Kristo kwa sababu ya miujiza Yake na ishara na maajabu, kisha akatofautiana Naye juu ya Maandiko, alikuwa baradhuli kutosha kuja na kumwambia juu ya jambo hilo. Roho yuyo huyo anaishi moja kwa moja katika mwalimu wa kidini leo. . .?. . . alichaguliwa na Mungu kuja kwenye hukumu hiyo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. "Watu wa kale, waliandikiwa tangu zamani hukumu hii, kubadili neema ya Bwana wetu kuwa ufisadi." Hiyo ni kweli kabisa. Katika Yuda, aya—aya ya 3 ya—ya Yuda, unaweza kupata jambo hilo. Hiyo ni kweli.

123 Angalia mambo hayo yote yakithibitika pale, ya kwamba kuna alama ya mnyama. Hapo ndipo ilipo. Kwa hiyo wakati unapokimbia hapa ukisema, "Vema, nitaonyesha wakati ile alama ya mnyama itakapokuja," jihadhari endapo wewe hujaipata tayari. Ndipo wale walio nayo, wataadhibiwa katika moto na kiberiti, uliomwagwa kutoka katika kikombe cha hasira ya Mungu, watateswa mchana na usiku, milele na milele. Ni jambo baya sana. Basi utaepukaje?

124 Kutakuweko na wakati, ambao unakuja sasa hivi. Angalia, katika shirika hili linaloshuka. . .Basi hebu niwape fununu ndogo hapa. Katika shirika hilo linaloshuka namna hiyo, unakuja wakati ambapo itakubidi kuwa mwana chama wa shirika hilo la sivyo huwezi kununua wala kuuza; ama kuwa na alama hiyo ya ukungeufu, alama ya kanisa. Huna budi kuwa mfuasi wa madhehebu fulani la sivyo huwezi kununua wala kuuza.

125 Basi, sikilizeni, ninyi watu mnaojua yaliyo Kweli. Mimi sisemi ondokeni kwenye kanisa lenu. Sisemi kitu dhidi ya ninino yenu. . .juu yenu ama wafuasi wenu. Ninazungumza juu ya makao makuu, huko nyuma wakati walipofanya kitu hicho madhehebu, na kuamua, "Tutafanya jambo *hili*. Tutafanya jambo *lile*." Nao wakafanya sheria hiyo kali sana. Naye Mungu anairarua vipande-vipande, na kulichukua Kanisa Lake moja kwa moja kutoka kule; daima alifanya jambo hilo.

126 Angalia katika safari ya wana wa Israeli. Wao waliwasha moto. Wakakaa kila usiku. Nguzo ya Moto ilining'inia juu yao. Nami sijali ulikuwa wakati gani wa mchana wala usiku wakati Nguzo hiyo ya Moto ilipoondoka, parapanda ililia nao Israeli wakafunga kambi wakaondoka. Kama ilikuwa usiku wa maname, saa nane alasiri, wakati wo wote ule, walifunga kambi

wakaifuata Nguzo ya Moto. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wao waliufuata ule Moto.

127 Vema, wakati Martin Luther alipoona Moto wa Mungu ukitoka, Martin Luther alitoka, akiufuata ule Moto huku anatoka katika Ukatoliki. Bali yeye alijenga chini kule kisha akafanya kanisa lake madhehebu, naye asingeweza kusogea mbele.

128 Moto uliondoka moja kwa moja, naye Wesley akauona Huo, naye akaufauta. Hiyo ni kweli. Moto wa Mungu ulimwacha Luther ameketi. Ndipo, muda si muda, Wesley akajenga chini Yake, kanisa la Methodisti la Kiwesley.

129 Kisha akaja Alexander Campbell, John Smith pamoja na Batisti, na kadhalika namna hiyo, na Moody, na hao wote. Ndipo, muda si muda, wakaanza kupata utaratibu, na kuwa wagumu, baridi, wakati yule nabii mzee alipokufa, na kadhalika. Kundi hili jipya likaja likiwa halina kitu ila elimu ya seminari, halafu, muda si muda, wapishi wengi wakaingia mle na kukiharibu kitu hicho.

130 Ndipo Roho Mtakatifu akatoka, nao Wapentekoste wakaliona wakatoka; sawa, wakatoka nje moja kwa moja, kutoka katika Methodisti na Batisti, na kadhalika. Sasa jambo lake la kuchukiza, bali ili kutimiza Neno la Mungu, Wapentekoste wakaunda madhehebu, nao wakawa baridi tu na wa utaratibu kama wengine wao. Lakini, angalia, hakutakuwa na wakati mwingine wa kanisa. Wakati wa Mwisho ni Wakati wa Kanisa la Laodikia, ambao si moto wala baridi. Wana dini ya kutosha tu, wakati muziki unacheza, kucheza huku na huko kwenye marefu ya kanisa, kisha wanaketi chini, wanaenda nyumbani na kuzungumza juu ya jirani yako.

131 Tunachohitaji sasa ni ufufuo wa mtindo wa kale uliotumwa na Roho Mtakatifu na Mungu, uliowaka moto, utakaokufanya ulale kifudifudi na kulia, usiku na mchana, na kulia na kuomboleza, na kupiga makelele, kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Tutafikia jambo hilo. Hiyo ni kweli.

132 Lakini hao hapo. Hapo ndipo hasa tulipofika, vuguvugu. Mungu alisema, "Inanichefua tumbo! Nitawatapika kutoka katika kinywa Changu." Hilo ni kanisa, kanisa la Kiprotestanti, limekataliwa. Kanisa la Kiprotestanti limekataliwa; tangu Pentekoste hadi Luther, kila sehemu Yake. Neno la Mungu husema hivyo.

133 Lakini kutoka katika kila moja ya makanisa hayo, Yeye amechukua Mteule. Yeye amechukua Mzao kutoka kila moja, kutoka katika Methodisti, Batisti, Presbiteri, Luteri, kote kote pale, Katoliki, na kadhalika. Yeye amechukua waliosalia, akatoa watu fulani nje.

134 Hapa si muda mrefu uliopita, maskini bibi mdogo aliyeketi papa hapa Louisville, Mkatoliki, akifa. Nilienda kule. Ndipo kasisi akasema, "Upuzi, kwa jambo kama hilo!"

Naye mumewe akasema, "Simile. Mwache aingie."

135 Nikaenda kule. Naye huyu mwanamke alipaswa kufa asubuhi iliyofuata. Nilipokuwa nikimwombea, ono likatokea, ndipo kasema, "BWANA ASEMA HIVI." Hiyo ni kweli. Asubuhi yake. . . Nikamwambia ingechukua masaa mangapi, kikamilifu kabisa, wakati angeenda nyumbani amepata afya. Wakacheka jambo hilo, kwa dhihaka. Basi saa hiyo hiyo aliyosema Roho Mtakatifu, akaenda nyumbani akiwa mwanamke mwenye afya, naye ni mzima leo. Yeye alikuwa Mkatoliki. Wao walikuwa Wakatoliki. Wao *walikuwa* Wakatoliki.

136 Unapopokea Nuru. . . Katika Agano la Kale. . . Hebu niwaonyeshe ile chapa sasa. Sikilizeni kwa makini, ndipo nitaingia moja kwa moja kwenye somo langu. Angalieni, katika Agano la Kale, wakati mtumwa alikuwa chini ya utumwa, halafu alikuwa na. . . Alinunuliwa kule, kwa bei fulani. Ilimbidi kumtumikia bwana wake mpaka kwenye mwaka wa yubile. Basi mwaka wa yubile ulipokuja, tarubeta ilipigwa.

137 Basi wakati huyo mtumwa alipokuwa huko nje, yeye na watoto wake, na mkewe na hao wote wakitaka kuyarudia makao yao ya zamani. Walikuwa wakifanya kazi ngumu mashambani, huku msimamizi akiwapiga, na *huku* na *huko*. Ndipo wakati kuhani wa yubile alipopitia kule, akipiga baragumu, na huyo kuhani kapiga baragumu, naye mtu huyo akasisikia ile baragumu. Yeye angeangusha jembe lake, angeacha cho chote alichokuwa anafanya, auangalie uso wa msimamizi wake, na kusema, "Huwezi kunipiga mara nyingine moja. Mimi ni huru." Aondoke aende moja kwa moja nyumbani. Kwa nini? Kuna kutangazwa kwa yubile, wakati wao walipoisikia ile sauti.

138 Na hiyo ndiyo Injili, yubile, ya kwamba wewe ni huru kutoka dhambini. Uko huru kutoka katika tabia hizo zote chafu na kadhalika ambazo ulimwengu umetoa hapa katika jina la dini, chini ya Protestanti na Ukatoliki, chini ya alama ya mnyama. Hiyo ni kweli. Uko huru.

139 Si lazima uwe hivyo. Lakini basi kama mtu huyo akikataa kuipokea hiyo, basi mtu huyo alitolewa hapo akapelekwa kwenye mhimili wa madhabahu ya kanisa, akatiwa alama, shimo likatobolewa kwenye sikio lako. Akawa mtumishi wa bwana huyo maishani mwake mwote.

140 Nawe ukikataa kuipokea Nuru ya Injili wakati imehubiriwa katika Nguvu za Roho Mtakatifu, na Biblia, unaweza kujitia muhuri kwa ajili ya kikomo chako cha milele. Amina.

141 Sasa angalia, jambo moja dogo, kama mtaniwia radhi kwa kutoa tamshi hilo muda kidogo uliopita, juu ya—juu ya huyo mtu. Lakini, angalieni hapa, "Kuwapoteza walio Wateule. . . "

142 Naam, tumekuwa tukiwapiga Waluteri, Batisti, na kadhalika, na Wakatoliki, sasa hebu niwaendee ninyi watu wa utakatifu kwa muda kidogo tu. Mnaona? Ninaamini katika utakatifu. Hamna budi kuwa watakatifu. "Pasipo utakatifu hakuna mtu atakayemwona Mungu." Si utakatifu wangu; utakatifu Wake. Na hakuna kitu ninachoweza kufanya juu yake; ni kile Yeye alichonifanyia. Usisimame njiani mwangu, maana sina wo wote, sijaribu hata kuwa na wo wote. Mimi sijaribu kuwa—kuwa.

"Unajaribu kushikilia, Ndugu Branham?" La, bwana.

143 Ninaachilia tu, na kumwacha Yeye ashikilie. Hiyo ni kweli. Yeye Ndiye anayeshikilia. Kaa tu ungali mfu, hilo tu ndilo unalohitajika kufanya. Jiweke tu mwenyewe mfu, Yeye atashikilia. Yeye tayari ameshikilia. Alishikilia pale hata akasema, "Imekwisha." Hilo lilimaliza jambo hilo. Mungu anatuacha sisi tufanye hivyo, vivyo hivyo. Imekwisha.

144 Lakini, enyi watu wa utakatifu, enyi Wanazarayo na Waprilgrim Holiness sasa, kumbukeni. Chini ya zile nguvu na kutoka katika kanisa la Wesley, ama kanisa la Methodisti, wakati walipounda madhehebu, enyi wapendwa wa utakatifu mlitoka, kasema, "Tutaendeleza utakatifu." Hilo ni zuri sana. Mliendeleza tu wakati huo, Wakati huo wa Filadelfia, mpaka ikafikia kwenye Laodikia. Lakini wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu ulipokuja, na ishara zikaanza kurudi kanisani, mliita jambo hili "Ibilisi." Kwa maana wao walinena kwa lugha na wakaamini katika mambo haya, mlisema, "Ilikuwa ni Ibilisi." Nanyi mlipofanya jambo hilo, mlimkufuru Roho Mtakatifu.

145 Ninawezaje kuuambia mkono wangu, "Sina haja nawe"? Kama kuna waalimu, kuna kunena kwa lugha. Kama kuna waijilisti, kuna karama za kuponya pia. Mguu unawezaje kuliambia jicho, "Sina haja nawe"? Mnaona? Ninyi, kama wewe ni mtoto aliyezaliwa na Mungu, unatembea na kukubali kwamba kila anachosema Mungu ni kweli. Utatembea moja kwa moja katika Nuru.

146 Wakati ulipofika kwa Kanisa kusogea, Luther alisogea. Wakati ulipofika kwa Kanisa kuusogeza mkono Wake, Wesley aliusogeza mkono. Wakati ulipofika kwa Kanisa kunena, Pentekoste ikajitokeza jukwaani. Hiyo ni kweli. Lakini, sasa, angalia.

147 Mnasema, "Na mfano?" Mnasema, "Kuna mfano wa jambo hilo?" Naam, bwana.

148 Mnatambua ya kwamba Yuda Iskariote, yule mpinga Kristo halisi, alikuwa mtu wa kidini sana? Mlitambua jambo hilo? Wao walikuwa na matumaini sana naye, hao ndugu, hata alikuwa mweka hazina wa kanisa.

149 Naye Yuda Iskariote alihesabiwa haki kwa imani, akiamini katika Bwana Yesu Kristo.

150 Alitakaswa kwa Neno. Waebrania, 17:17... Ninamaanisha, Yohana 17:17, "Uwatakase, Baba, kwa ile Kweli; Neno Lako ni Kweli." Naye alikuwa Neno.

151 Nao walipewa nguvu kwenda kuihubiri Injili, na kuwatoa pepo, na kuwaponya wagonjwa. Yuda Iskariote, Mathayo 10, alitajwa miongoni mwao. Nao walitoka wakaenda wakawatoa pepo, na kuihubiri Injili hivi kwamba wenye dhambi walitubu na pepo wakatoka. Nao wakarudi wakifurahi na kupiga makelele, wakiwa na wakati mkuu, mkutano mdogo wa kambi, wa utakatifu. Naye Yuda alikuwa moja kwa moja pamoja nao. Hiyo ni kweli kabisa, aliambatana nao moja kwa moja.

152 Bali ulipofikia wakati wa Pentekoste, Yuda lionyesha alivyo hasa.

153 Hapo ndipo kanisa la utakatifu lilionyesha lilivyo hasa, papo hapo, nalo likageuka moja kwa moja na kukana Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa anawaongoza kwenye Maji yenye kilindi; wakageuka moja kwa moja na kumkana Yeye. Najua wana wingi wa washupa-...

154 Mimi si Mpetenkoste. Mimi sijakuwa mfuasi wa madhehebu yo yote ya Kipentekoste, la hasha. Nimesimama katika pengo. Mimi si Mpentekoste, Methodisti, Batisti. Mimi ni Mkristo tu wa Biblia. Hivyo tu. Ninaamini Neno lisemavyo. Wala siwezi kukana karama ya kunena kwa lugha; nikifanya hivyo, nitakana kufundisha na kila karama nyingine iliyo na uvuvio. Hiyo ni kweli. Sijakubaliana kamwe na ndugu wa Kipentekoste juu ya "ushuhuda pekee," wa kunena kwa lugha. Mimi sifanyi jambo hilo. Naam, hiyo ni kweli, kama wao wakiliamini namna hiyo. Hiyo ni kazi yao, mnaona, lakini hiyo ni sawa kabisa. Mimi... Paulo alisema, "Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha." Ningetaka kumwona kila mtu akiwa karibu namna hiyo na Mungu.

155 Wao wana miigo mingi, imani nyingi haramu. Wametoka huko nje, mara nyingi, na kufanya kama kwamba wana Roho Mtakatifu, na kusema kitu ambacho hakikuwa kunena kwa lugha. Maisha yao yalithibitisha ilikuwa ni kitu gani. Bali kumekuwa na kitu halisi kikiendelea vile vile, wakati wote.

156 Vema, mbona Ibilisi asitupe rafiki msiri, chambo cha kunguru? Hakika, angeweza, kujaribu kuzuia. Yeye alitupa kitu kile kile katika utakatifu. Alitupa kitu kile kile katika Methodisti. Alitupa kitu kile kile katika siku za Luther. Naye anatupa kitu kile kile leo. Na chini ya nguvu za karama, za kuponya Kiungu na upambanuzi, yeye anatupa kitu kile kile nje.

157 Lakini kitisha ndege kina maana gani kwako, kama ungeweza kuzungumza lugha ya ndege? Ndege wanasema, "Ninapoona kitisha ndege, hicho ni riziki halisi." Matofaa mazuri sana yaliyopo, yako moja kwa moja karibu na mahali

ambapo rungu zote zimewekwa na vitisha ndege vinaning'inia. Hiyo ni kweli.

158 Lakini mnaona jinsi roho huyo alisogea moja kwa moja huku. Basi Yesu aliangalia na kuona jambo hilo kimbele kupitia kanisa Katoliki, likitoka. Kasema, "Msimwite mtu ye yote baba. Msipayukepayuke, mambo haya yote." Katoka kasema, "Sasa iweni waangalifu, mpinga Kristo atafanana sana hata jambo hilo litawapoteza walio Wateule kama yamkini."

159 Angalia, ndugu, ni bikira wangapi waliotoka kwenda kumlaki Bwana? Kumi. Wote walikuwa bikira. Maana ya *kutakasa* ni nini? "Bikira msafi, mtakatifu." Kumi kati yao walikuwa bikira. Watano hawakuwa na Mafuta katika taa yao. Watano walikuwa na mafuta katika taa yao. *Hawa* watano walikuwa watakatifu tu na bikira kama *hawa* walivyokuwa. Lakini *Mfuta* yanawakilisha kitu gani, katika Biblia, mahali tulipolichukua jambo hilo jana usiku, usiku wa juzijuzi? Roho, "Roho Mtakatifu." Wao walijisafisha kisha wakaketi pale, bali waliogopa wakasimama mbali na Chemchemi iliyomwaga yale Mafuta. Mnaona, wakajiundia madhehebu kisha wakatulia, nao hao, wenye uvuguvugu. Huko ndiko ule wakati wa kanisa ulikoelekea.

160 Naam, sasa tunakuja kwenye alama ya Mungu. Nina dakika thelathini, Bwana akipenda. Sasa nawatakeni mfungue pamoja nami, kwanza, tuone jinsi ilivyo mhimu, alama hii ya Mungu.

161 Kumbukeni alama ya mnyama ni nini; si ukomunisti. Alama ya mnyama inatoka Rumi, kila mahali ulimwenguni; Ukatoliki, huku Uprotestanti umejiingiza ndani yake, dini halisi. Nao wataunganisha makanisa yote mpaka kila kanisa litapaswa kukubaliana na kitu hicho, ama hao wetu wasio wa kimadhehebu watatupwa kando. Hiyo ni kweli.

162 Ufunuo sura ya 9 sasa. Hebu tusome kwa makini sana hapa kwa muda kidogo, Mungu akipenda, tuone kile alichosema katika Neno Lake. Sasa... [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] ...ya—ya Ufunuo, na sura ya 4. Sikilizeni jambo hili.

> *Wakaambiwa* (walipoona yale mapigo yakimwagwa) *wasiyadhuru majani* wala miti...*wala kitu cho chote kilicho kibichi, wala mti wo wote, ila*...*watu wasio na muhuri ya Mungu katika vipaji vya* uso wao.

163 Wakati yale mapigo yalipokuwa yanakuja, kitu tu kilichokuwa kimekingwa kilikuwa ni wale waliotiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu. Hii ndiyo hukumu ya kuchunguza, wakati watu...Na iwapo Mungu atanisaidia, katika dakika chache mtaona jambo hilo kwa Neno la Bwana, ya kwamba huu ndio wakati wa kutia muhuri mahali hapo. Na hao watakaoikataa Hiyo, hakuna kilichosalia ila adhabu ya Milele.

164 Sasa tufungue kwenye Agano la Kale. Basi hebu tufungue hapa, mkiweza, kwenye Kitabu cha Ezekieli, mkiweza, na

tusome kidogo katika Ezekieli 9. Naam, kwa neema ya Mungu sasa, naomba atusaidie. Nasi tutulie sasa kwa kufundisha, kwa dakika thelathini tu zifuatazo, Mungu akipenda. Sasa jambo hili linahusu, huku mkiliandika, Ezekieli 9, hili linahusu . . .

165 Jambo la kwanza tunalopaswa kuamua sasa, Muhuri ya Mungu ni nini? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hamfikiri jambo hilo lingekuwa muhimu sana? [Kusanyiko, "Amina."] Je! Bablia ni Neno zuri kutosha kwa ajili yenu? Sasa najua mna kitu hicho, wale wanaosema, "Kuadhimisha siku ya sabato," lakini hakuna fungu moja la Maandiko kuunga jambo hilo mkono, katika Agano Jipya. Hebu tuone Muhuri ya Mungu ni nini, bila shaka. Fungueni Waefeso 4:30, 4:30, na 1:13. Yaandikeni. Waefeso 4:30 inasema:

> *. . .msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi.*

166 Basi, maana ya *kutia muhuri* ni nini? Kutia muhuri ni "ishara ya kukamilika." Sivyo?

167 Vema, mlipata kuona mwana reli akipakia mabehewa? Yeye atatoka aende na ataweka kiasi fulani *hapa*, na kiasi fulani *hapa*. Mkaguzi anapita pale, anaangalia ndani; na iwapo *hili* limelegea kidogo, linatikisika, "La. Mimi sitalitia muhuri. Sina budi kulifungua na kulirudia tena." Basi, atajaribu kulipakia tena; atakosea hili. Mkaguzi anapita pale, "Ni makosa. Fanya tena."

168 Na hivyo ndivyo Mungu amekuwa akifanya na kanisa Lake kwa muda mrefu. Utapakiwa, nawe unaenda Mbinguni; unachukua kila kitu. Karata zako, a-ha, kila kitu kingine unachoweza kupakia kwenye kanisa, unajaribu kwenda nacho. Mungu anahukumu jambo hilo; huko tayari kwa kutiwa mhuri.

169 Lakini wakati Mungu anapomwona mtu, mwenye roho iliyopondeka, iliyovunjika, moyo mwaminifu, kwenye madhabahu, Mungu hufunga mlango wa ulimwengu kwake, na kumtia muhuri mle kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, na unadumu mpaka Yesu atakapokuja; si kutoka ufufuo mmoja hata mwingine, lakini, "hata siku ya ukombozi wako."

170 Wakati behewa hilo, mlango, unapofungwa, na muhuri wa serikali umewekwa kwake, haliwezi kufunguliwa tena mpaka litakapofika linakokwenda.

171 Na kila mtu aliyezaliwa mara ya pili na kutiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu, hana tamaa tena ya ulimwengu hata siku Yesu Kristo atakapomwingiza katika ule Ufalme. Kwa hiyo kama una shida, na kusema una Roho Mtakatifu; ama wewe ni mfuasi wa kanisa la Methodisti, kanisa la Kibatisti, kanisa la Kipentekoste; ama ulipiga makelele, ukanena kwa lugha; ukabatizwa kifudifudi, kichalichali, ukanyunyiziwa; kama ungali unapata shida za namna hiyo, afadhali urudi ukachunguze ule mzigo. Hiyo ni kweli. Umechukua mzito

sana; umelegea mno, unatikisika. Mungu hatalitia muhuri namna hiyo.

172 Wakati chembe ya ngano inapoanguka ardhini, haidhuru . . . Kama chembe hiyo ya ngano ikifa kwa nafsi yake, haiwezi kuzaa gugu, kuokoa nafsi yake. Chembe ya ngano itazaa chembe ya ngano, hakika kweli. Na kama tumepandwa kwa Mbegu ya Mungu isiyoharibika, Hiyo inawezaje kuzaa cho chote ila uhai wa Maisha ya Kristo?

173 Roho Mtakatifu akiliongoza Kanisa, analiongoza Hilo kwa Nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo, nawe umetiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Hiyo ni Biblia. "Msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Waefeso 4:30.

174 Naam, kabla ya Roho Mtakatifu kuja, yeye ametiwa muhuri kabla ya wakati wa Mataifa kuanza. Ametiwa muhuri chini ya hivyo vinara vya taa vya dhahabu, (tulikuwa na mchoro, kulipata), kule nyuma kwenye wakati ule.

175 Yeye aliendelea kucheza-cheza nao kote kote kupitia kwa Ibrahimu, Isaaka, Yakobo, Daudi, na kote kote kupitia ule wakati wa giza waliokuwa nao katika siku za Ahabu, na kuendelea, Sulemani, na kadhalika, hata ikatokea kwenye ile hali ya uvuguvugu. Lakini kabla tu Yeye hajafunga majira hayo pale, alitoa uweza mkuu wa Roho Mtakatifu kwa Wayahudi peke yao, "Msiende kwa Mataifa, bali enendeni kwa kondoo waliopotea wa Israeli." Sivyo? "Alikuja Kwake, wala walio Wake hawakumpokea."

176 "Bali hao waliompokea, aliwapa Uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu." Yeye alisema, "Ninawapa Uzima wa Milele." *Uzima* wa Milele unatoka kwenye neno la Kiyunani la "Zoe." Zoe ni Uzima ule. Zoe ni Uzima wa Mungu. Basi kama Uzima wa Mungu unaishi ndani yako, unatoa maisha ya kitaua hakika tu kama vile ninavyosimama kwenye jukwaa hili. Na mtu aliye nao Huo, hawezi kuangamia kama vile Mungu asivyoweza kuangamia, kwa maana Mungu yumo katika huyo mtu. Amina. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni; bali yuna Uzima wa milele." "Yeye ailaye nyama Yangu na kuinywa Damu Yangu, nitamfufua katika siku ya mwisho." Hilo ni Neno Lake. Ni faraja jinsi gani kwa mwamini! Na ni hukumu jinsi gani kwa wale wanaokataa kutembea katika Nuru.

177 Inakuwa joto, sivyo? Vema, Hilo ni nzuri kwenu. Angalieni, angalieni kama jambo hili ni kweli. Ndugu, tungelichukua, Andiko baada ya Andiko, juma baada ya juma, juma baada ya juma, na kukaa kwenye jambo hili, moja kwa moja . . . somo lile lile, kwa mwaka mmoja, na hata hivyo tusitoke kwenye Biblia, yote, na moja kwa moja kwenye jambo lile lile.

178 Sasa kwa ajili ya utangulizi mdogo tu hapa, tutarudi nyuma tuone kuukataa ubatizo wa Roho Mtakatifu kuna maana gani kwako, kile ulichomaanisha kwao kwenye siku ile.

179 Naam, katika Ezekieli sura ya 9, huyo nabii aliiona Yerusalemu. Sasa kumbukeni, tunazungumza juu ya muda huo pale, Wayahudi, kabla tu ya kuisha kwao.

180 Sasa sisi tuko katika Mataifa, wanakoishia. Ndipo tutaingia katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Vema.

181 Lakini sasa angalia, mnawamalizia Wayahudi sasa. Nabii aliona jambo hilo kimbele. Hii ingali ni miaka mia, yapata miaka mia nane, kabla ya kule kuja kwa Bwana, nayo yalitabiriwa na nabii. Sasa sikilizeni kwa makini tunaposoma.

> *Kisha akalia kwa sauti kuu maskioni mwangu, akisema, Waamuru wale wanaousimamia mji wakaribie,* na *kila mmoja na awe na* silaha ya kuua ama *kitu chake cha kuangamiza mkononi mwake.*

182 Sasa angalieni kwa makini sasa tunaposoma.

> *Na tazama, watu sita wakaja, wakitokea*. . .*njia ya lango la juu*, linaloelekea *upande wa kaskazini, kila mmoja ana kitu chake cha* kuangamiza *mkononi mwake; na mtu mmoja kati yao*, mwenye mavazi meupe, *amevaa bafta, naye ana kidau cha wino cha mwandishi kiunoni. Wakaingia,*. . .*kasimama* mbele, *karibu na madhabahu ya shaba.*
>
> *Na huo utukufu wa Bwana wa Israeli ulikuwa umepanda juu kutoka kwa kerubi, ambaye ulikuwa juu yake, mpaka kizingiti cha nyumba; akamwita mtu yule aliyekuwa amevaa bafta, mwenye kidau cha wino cha mwandishi kiunoni.* (Sikilizeni.)
>
> *BWANA akamwambia, Pita kati ya mji, kati ya Yerusalemu* (Wakielekea Yerusalemu), *ukatie alama katika* kipaji *vya nyuso vya watu wanaougua*. . .*na kulia kwa sababu*. . .*machukizo*. . .*yanayofanyika kati yake.*
>
> *Kisha* basi *hao wengine aliwaambia, nami nikasikia, Piteni kati ya mji nyuma* yao, *mkapige;* na *jicho lenu lisiachilie, wala msione huruma;*
>
> *Waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana,*. . . *watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu ye yote* ambaye. . .*hiyo alama; tena anzeni katika patakatifu pangu.* Na. . .walianzia *kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba.*

183 Sasa mwangalie huyo nabii katika Roho, alipandishwa Utukufuni. Mungu akasema, "Nitakuonyesha jinsi nitakavyolitatua jambo hilo na Wayahudi, kabla ya kuja kwa Mataifa." Someni aya hiyo, ama sura inayotangulia. Naam,

alipoingia pale, alisema, "Nikaona..." Kwanza, yeye aliona dhambi katika mji, mfano wake hajaona hapo awali, kisha akaona Yerusalemu. Sasa kumbuka, ulikuwa ni kikomo cha Wayahudi tu, sio Mataifa; Wayahudi, na mji wao mkubwa, Yerusalemu. Kama tu jana usiku, tulikuwa tumelielekeza kwa Waprotestanti; naam, usiku huu, tunalielekeza kwa Wayahudi. Yeye alisema, "Piteni kati ya mji." Hapa wanakuja watu wenye vitu vya kufisha mkononi mwao, wakitoka kwenda kuua kila kitu mjini. Akasema, "Sasa acheni tu, kwa muda kidogo tu."

184 Na kutoka kule akaja mtu aliyevaa mavazi meupe. Hebu tusimame kidogo. "Amevaa mavazi meupe," haki, utakatifu. "Amevaa mavazi meupe," Ambaye alikuwa na kidau cha wino kiunoni mwake. Yeye alisema, "Piteni kati ya mji kwanza, kabla wao hawajakuja, mkawatie alama katika kipaji cha uso, alama katika kipaji cha uso cha kila mwanamume, mwanamke, mvulana, na msichana, katika mji, anayeugua na kulia kwa sababu ya machukizo yanayofanyika mjini, kwa ajili ya dhambi za watu." Watie alama!

185 Kisha, baada ya Yeye kupita na kuwatia alama, alirudi akasema, "Imekwisha."

186 Ndipo akawatuma wale watu, kasema, "Piteni, msiachilie cho chote, bali muangamize kabisa cho chote kisicho na alama hiyo juu yake."

187 Angalia hapa, ndugu. Mtia alama yule hakuwa mwingine ila Roho Mtakatifu.

188 Basi angalia, kama Yeye akija Jeffersonville, usiku huu, kwenye Maskani ya Branham, ama maskani mengine yo yote mjini, ama kanisa lingine lo lote, angetia nani alama, aliyekuwa mwaminifu sana na wa kweli mbele za Mungu hata walilia na kuomboleza, na kuomba mchana na usiku, kwa ajili ya dhambi za mji? [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani mara mbili—Mh.]

189 Angewafanyaje wahubiri wanaowaachilia wanawake wao watoke nje na mavazi ya kuogelea, na kujinyosha katika kaptura, na kutembea huku na huko mitaani; na kuimba katika kwaya, na kujipodoa na kutenda kama Mayezebeli. Na wakati...Wanaume huko nje, wakivuta sigara, na kunywa pombe, kufanya yasiyofaa, na kucheza karata, cho chote kile! Nao wanafanya kama kwamba hawajali jambo hilo; wakienda kwenye chakula kikubwa cha jioni cha kuku, ama karamu mahali fulani. Wanakaa nyumbani Jumatano usiku na kuangalia televisheni, badala ya kuhudhuria mkutano wa maombi. Katika wakati wa kiangazi, wanafunga kanisa, wasiwe na ibada. Yeye angetia nini muhuri?

190 Tunachohitaji, usiku wa leo, ni kukaba baadhi ya uijilisti huu hapa wa Hollywood! Na ufufuo wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu, wanaume na wanawake wanaoshuka

kwenda madhabahuni! Na kuacha huku kuwapa mikono, na kuwashika mikono, na kuwanyunyizia, na kuwabatiza kifudifudi, kichalichali, na taratibu hizi zingine zote ndogo na itikadi. Nao washuke kwenye moyo uliopondeka na kuvunjika kabisa, mahali palipo na dhambi. Wachanganyishe hayo pamoja, na kuanza mlio wa mtindo wa kale, wa mwana aliyezaliwa. Amina. Hao ndio wanaompata Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

191 Haidhuru kama wao ni Methodisti, Batisti, ama Wakatoliki, ama wo wote wale! Wanapofika kwenye yale madhabahu na kulia, usiku na mchana, "Ee Mungu, angalia dhambi ya mji huu! Moyo wangu hauwezi kupumzika! Siwezi kupumzika, Bwana, kuona mambo haya yanayoendelea. Ee Mungu, fanya jambo fulani! Tutumie ufufuo wa mtindo wa kale," uko kwenye mpaka wa kumpata Roho Mtakatifu basi, ndugu! . . . ? . . .

192 Lakini kama ukitembea kwenda kule kwa sababu umeruka juu chini, ama kwa sababu umecheza dansi na muziki, ama kwa sababu umefanya jambo jingine; na umetembea kila mahali na kushikwa na hasira, wala hujali, na kuruka kwa ghafla, na kuzozana, na kujiunga na kanisa, na kuruka kutoka mahali pamoja hata pengine; inaonyesha ya kwamba hukupata kitu hapo awali.

193 Ndugu, hiyo, hiyo ni dawa nzuri na kali, lakini itawapa afya. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Itawatoa, bila aliye mnyonge miongoni mwenu.

194 Kama Musa. Ningetaka kuangalia katika mfuko wake wa dawa, nanyi je? Yeye alikuwa na watu milioni mbili huko nje. Mngetaka kuangalia katika mfuko wa Musa wa dawa, kile ulichokuwa nacho? Wote wakiwa wazee, na mamia ya watoto wachanga waliozaliwa kila usiku, na watu waliolemaa, na wagonjwa. Naye alipotoka, katika miaka arobaini, hapakuwapo na hata mmoja—mmoja aliye mnyonge kati yao. Hivi wengine wenu madaktari, mlioketi hapa usiku wa leo, msingetaka kuangalia katika mfuko wake wa dawa?

195 Hebu tuungalie mle ndani tuone ni nini. Sasa angalieni kule nyuma. Tutaona. "Mimi Ndimi Bwana akuponyaye." Jambo ndilo hilo. "Amina." Hivyo ndivyo ilivyokuwa. "Mimi Ndimi Bwana akuponyaye." Kasema mtoto atazaliwa. "Mimi Ndimi Bwana ukuponyaye." Ana nimonia. "Mimi Ndimi Bwana akuponyaye." Hiyo ndiyo dawa tu angaliweza kutoa. Ndiyo tu aliyohitaji. Ndiyo tu aliyokuwa nayo. Hiyo ndiyo Mungu aliyompa.

Bila shaka, leo, "Hatuamini katika jambo Hilo. La, hilo . . . "

196 Mungu habadiliki. Yeye ni yeye yule. Kama roho hii, watu wakifanya yasiyofaa wanavyofanya leo, chini ya jina la Ukristo, ilimfanya Mungu kuchefuka tumboni kule nyuma, ilikuwa ni "chukizo" kwa watu kufanya hivyo, ni chukizo leo. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Loo, ninajisikia wa kidini.

197 Angalia, "Nenda kule," Yeye akasema, "pita katika mji ukatie alama juu yao waonaougua na kulia kwa ajili ya chukizo linalofanywa katika mji." Kisha akasema, "Baada ya kufanya jambo hilo," Yeye aliwatuma watu hawa wenye upanga wa kufisha, nao wakatoka wakaenda na kuua kila kitu.

198 Naam, ewe mwana historia, hebu kidogo. Yesu alikuja katika mwili; Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili. "Mugu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Na wakati alipokuja katika mwili, alienda kila mahali akifudisha. Wao walimwita "Beelzebuli," mpiga ramli. Walimfanyia mzaha, juu ya kuzaliwa Kwake, cho chote kile; wakamkataa, wakamtupa nje.

199 Yeye alisema, "Yeye atakayesema neno juu ya Mwana wa Adamu, atasamehewa, bali yeye atakayesema juu ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao."

200 Yeye aliwakusanya Wayahudi wachache pamoja. Hakwenda kwa Mataifa. Alienda kwa Wayahudi. Alitumwa kwa Wayahudi; haikuwa majira ya Mataifa. Mshumaa wa mwisho ulikuwa unawaka kwenye wakati wa Wayahudi, Naye akaenda kule. Na kulikuwa na watu wachache waliompokea, walioitwa watoke.

201 Kama tu vile ilivyo leo. Kama tu vile Roho Mtakatifu akinena katika Yesu Kristo, alivyowaita wakati huo; vivyo hivyo Roho Mtakatifu ananena katika Yesu Kristo, akiita, leo.

202 Wao waliamini ya kimbinguni. Walimwangalia Kiongozi wao. Walimwangalia. Wao walijua Yeye alikuwa mfalme wa manabii. Walijua cho chote alichokuwa. Yale aliyonena, Mungu aliyathibitisha na kusema yalikuwa ni Kweli. Wao walijua walikuwa na ile Kweli. Walijua ni Nani waliyekuwa wanamwamini, nao wakapiga hatua pamoja na Yesu.

203 Ndipo wakamsulubisha. Akasema, "Baba, wasamehe, hawajui watendalo."

204 Bali Siku ya Pentekoste ilipotimia, kulikuwa na kundi ndogo la watu, wanaolia na kuomboleza na kuendelea. "Bali ilipotimia Siku ya Pentekoste . . . "

205 Mara kasisi akaja barabarani, akiwa na saduku la mkate mwembamba, saduku la ushirika, kasema, "Toa ulimi wako sasa, nami nitakunywa divai"? Ni upuzi namna gani! Moja kwa moja akaja mhubiri wa Kiprotestanti, akasema, "Tutachukua mkono wa kuume wa ushirika, kisha tuchukue miezi sita ya makatazo"? A-ha! Upuzi! "Nitawanyunyizia. Nitawabatiza. Nitawachukua upande *huu*, na kuwachukua kanisani, niwape mkono wa kuume wa ushirika"? Upuzi!

206 "Bali Siku ya Pentekoste ilipotimia, kukaja ghafla toka Mbinguni kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Ndimi

zilizogawanyika zikawakalia, kama moto." Wakaanza kutatarika, kupayukapayuka, kutoa mate, na kutema mate, na kuendelea.

207 Mnasema, "La!" Nitawathibitishia kwa Biblia. Naam, bwana. "Unataka kuniambia hivyo ndivyo walivyofanya?" Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema.

208 Je! mlijua Isaya alitabiri? Hebu niwasomee kitu kidogo kutoka kwa Isaya hapa, kwa muda kidogo tu. Isaya, sura ya 28, kuanzia aya ya 8.

> *Maana meza zote zimejaa matapiko*. . . (akinena juu ya siku hii). . . *na uchafu, hapana mahali* pasafi. (Ndugu, kama hiyo haikuwa ni picha ya Myahudi!)
>
> *Atamfundisha nani maarifa? atamfahamisha nami habari hii*? (tunazungumza juu ya Fundisho, usiku huu) . . . *Je! ni* hao *waliachishwa maziwa*, hao *walioondolewa matititini?*
>
> *Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni*;. . . (hivyo ndivyo Injili inavyokuja, kutoka Mwanzo mpaka Ufunuo!)
>
> *La, bali kwa midomo ya watu wageni na* pamoja na *lugha nyingine atasema na watu hawa;*
>
> . . . na *hii ndiyo raha yenu*, amani niliyosema ingekuja. Na kwa haya yote wasingesikia, bali wakaondoka, wakitikisa kichwa chao.

209 Naam basi. Hivyo ndivyo alivyosema. Hilo halikuwa neno langu; hilo ni Neno Lake. Chagueni, mkiweza. Haliwezi kubadilishwa. Yeye alisema, "Amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo na pale kidogo." Injili yote haina budi kutolewa.

210 Injili yote haina budi kuanza hapa, nao waliihubiri. Nao walipofanya jambo hilo, Nguvu za Roho Mtakatifu zikaja.

211 Na hao Wayahudi walikuwa wamemfanyia Yesu mzaha, lakini walicheka, wakasema, "Ha-ha-ha! Watu hawa wamejaa divai mpya." Walitia muhuri kikomo chao cha Milele. Wakasema, "Imekuwaje basi kwamba tunaweza kusikia katika lugha yetu wenyewe, kazi za ajabu wanazonena? Mbona, watu hawa wamejaa mvinyo mpya. Ha-ha!" Wao wakafanya mzaha na kucheka.

212 Ndipo Petro, maskini mtakatifu yule anayejifingirisha, mhubiri wa barabarani ameketi kwenye jukwaa la barabani anarukaruka juu yake. Kasema, "Enyi watu wa Uyahudi, nayi mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkaisikilize sauti yangu. Lakini jambo hili—jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli. Watu hawa hawajalewa kwa mvinyo mpya, kama mnavyodhania, kwa maana ni saa tatu mchana. Bali

jambo hili ni Lile." Yeye alielekeza kwenye Biblia. Mara nyingi nimesema, "Kama jambo hili si Lile, mimi nitaweka tu hili mpaka Lile lijapo, kama kuna kitu cho chote tofauti." Sawa. Kasema, "Jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli. Itakuwa katika siku za mwisho," miaka elfu mbili iliyopita.

213 Miaka ya kwanza elfu mbili, ulimwengu uliangamizwa kwa maji. Miaka elfu mbili iliyofuata, Kristo akaja. Katika miaka elfu mbili ya mwisho, nitaimwaga Roho Yangu." Haleluya! Si "Nitawaelimisha wahubiri fulani na kutuma makasisi fulani."

214 "Lakini nitamwaga Roho Yangu kutoka Mbinguni; wana wenu na binti zenu watatabiri; juu ya watumishi wangu wa kike na wa kiume nitamwaga roho Yangu, nao watatabiri. Nitatoa ishara katika mbigu juu, na nchi chini." Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Huo ulikuwa ni mzinduo.

215 Nao hao Wayahudi wakacheka na kufanya mzaha, na kusema, "Wao wamejaa mvinyo mpya." Jambo hilo lilitia muhuri kikomo chao.

216 Katika A.D. 96, kuja kwa Titus, akishuka kutoka ile sehemu, Yerusalemu ilizingirwa na majeshi. Basi mnajua kilichotukia? Hao Wayahudi walisema, "Sasa tutarudi katika nyumba ya Bwana."

217 Bali hao walioonywa na kujazwa na Roho Mtakatifu . . .

218 Kama alivyosema Josephus, "Hao watu kama wala watu, mmekuwa mnakula mwili wa Yesu wa Nazareti." Kasema, "Waliuficha mwili Wake, nao wamekuwa wakiula." Wao walikuwa wakila ushirika. Kasema kwamba wao, kundi hilo huko nyuma, "Hao wazushi."

219 Mnajua hao watu huko yuma walikuwa wanaitwa "wazushi"? Mnajua jambo hilo? Mnajua *wazushi* ni nini? Mtu ambaye ana "kichaa." Naam. Mwangalie Mtakatifu Paulo.

220 Naam, ninyi watu, ninyi—niyi Wabatisti mnapenda kusema, "Mtakatifu Paulo, loo, ninamwamini." Ninyi Wakatoliki mnasema, "Loo, Mtakatifu Paulo," kisha mnabusu hata mnaimaliza miguu yake miwili mitatu, hizo sanamu kule Rumi. "Mtakatifu Paulo! Naam, bwana!"

221 Angalia aliyosema Mtakatifu Paulo alipokuwa mbele ya Agripa. Alisema, "Katika njia wanayoiita uzushi," mtakatifu anayejifingirisha, "hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu." Amina.

222 Ningalitaka kumuunga mkono; nigesema, "Ninaamini vile vile, Paulo! Haleluya! Naam, bwana, jambo lile lile! Miaka elfu moja mia tisa imepita, Paulo. Ningali ninaamini jambo lile lile!" Ningali nina Roho Mtakatifu; ishara zile zile, maajabu yale yale, kila kitu vile vile; wakiendelea tu, Roho Mtakatifu yule yule, tungali tumetiwa muhuri hata (lini?) siku ya ukumbozi.

223 "Injili hii itahubiriwa..." Nini? "Injili!" Injili ni nini? Si "Neno tu." [Ndugu Branham anagongagonga mimbara mara nne.] Paulo alisema, "Injili ilitujia sisi, si kwa Neno tu, bali kwa Nguvu na dihirisho la Roho Mtakatifu ndivyo Injili ilivyokuja." [Brother Branham anagonga mimbara mara tatu.]

224 Paulo alisema, "Sikuja na baadhi ya elimu ya seminari, nikaja nikitoa maneno makubwa yenye ufasaha, ili kwamba wokovu wenu uwe na msingi juu ya maneno makuu mno na midomo yenye ufasaha, na baadhi ya nyimbo fulani za kidini ama imani ya mitume, ama kitu kama hicho. Mimi sikuja kwenu namna hiyo. Bali nilikuja kwenu nikijua jambo moja tu, Nguvu za kufufuka Kwake Yesu Kristo, na madhihirisho ya Roho Mtakatifu." Haleluya! Mungu na atupe Paulo wengine, wenye ngumi kubwa zenye nguvu ambazo zinaliweka Hilo kule pamoja na Inji-. . . bila kushindiliwa mambo fulani na seminari. Amina. Muhuri ya Mungu! Amina.

225 Naam, tuna muda gani? Mwingi sana, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hivyo ndivyo nilivyodhani. Hilo ni sawa. Kesho ni Jumamosi, hakuna mmoja wenu hafanyi kazi. Vema. Vema. Kumbukeni, da—dakika chache tu.

226 Ombeni! Angalia, ndugu, huu ni wakati wenye uchaji. Huu ndio wakati tunaopaswa kuwa tukitoa hesabu. Sisimami hapa nikijifanya mcheshi. Kama nilikuwa hivyo, ningeenda madhabahuni na kutubu. Huenda ninatenda kama mcheshi kwa wengine wenu, bali simaanishi kuwa hivyo. Ninatenda kipumbavu kidogo, mara kwa mara; siwezi kuzuia jambo hilo. Kitu fulani kinaniingia, kinanifanya nitende namna hiyo, kwa hiyo siwezi kuzuia jambo hilo. Lakini moyoi mwangu, ndugu, ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote. Kwa miaka ishirini na kitu nimehubiri Hili kwenye mimbara hii, kila mahali ulimwenguni, kisha Mungu akathibitisha jambo hilo kwa ishara na maajabu. Amina. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Naam.

227 Sasa Yeye alisema, "Waamuru walio na silaha wakaribie." Wao walikataa kuipokea alama ile. Ndipo akaenda, naye Titus akaziteka kuta za Yerusalemu, nao wakakimbia mjini; wakawafanya wafe kwa njaa mle ndani, hata wakawachemsha watoto wao kwa wao na kuwala. Walikula maganda ya miti, nyasi ardhini. Kisha hatimaye ilipowabidi kujisalimisha... Titus, alipoingia Yerusalemu, aliangamiza kila kitu mle ndani, akawaua wanawake, watoto, watoto wachanga, makuhani, cho chote kile, kisha akauteketeza huo mji.

228 Naye Yesu alisema, "Wakati unakuja ambapo halitasalia jiwe hata moja."

229 Kasema, "Angalia kanisa letu kuu mno la jimbo. Ndugu, sisi ni Batisti, ama Methodisti, ama Pentekoste, ama cho chote kile."

Akasema, "Halitasalia jiwe juu ya lingine."

230 Inaoyesha ya kwamba "Mungu haishi katika nyumba iliyojengwa kwa mikono." Mungu huishi katika mioyo ya wanadamu. "Kwa maana Wewe umeniandalia Mimi mwili." Roho Mtakatifu haishi katika nyumba. Anaishi moyoni. Huo ndio hekalu. "Hamjui kwamba ninyi ni hekalu za Mungu aliye hai?" Amina. Kujenga hekalu, kujenga kanisa, imani yako yote imejengwa juu ya hekalu lako ama kanisa lako, sanamu ya mbao, huku unachukua alama ya mnyama wala hujui. Hiyo ni kweli. Ukirukaruka na kutumia wakati wako wote, wahubiri, kuyasaidia madhebu yako, huku wanaenda moja kwa moja jehanamu pamoja nayo wawezavyo kwenda.

231 Ninakwambia, ndugu, wakati umefika kwa wanaume kuamka na kuhubiri kwa Nguvu za Roho Mtakatifu, wakati kila mahali, hebu tuwaite Methodisti, Batisti, Presbiteri, Katoliki, na kadhalika, wavuke waje kwa Yesu Kristo.

232 Naam, unasema, mchungaji wa kale alibeba asali, akaiweka mwambani. Wakati kondoo aliye mgonjwa alipoiramba, alipata afya.

233 Ndugu, nina mkoba mzima uliojaa hiyo hapa, usiku huu. Nami nitaiweka kweye yule Mwamba, Kristo Yesu, ndipo kondoo wagonjwa waweze kuiramba wapate afya. Hiyo ni kweli. Ndugu, sikiliza, sitaiweka kwenye kanisa lo lote. Si ya kanisa lo lote. Ni ya Kristo. Hiyo ni kweli kabisa.

234 Wa kawaida! "Loo, naam, tunamwamini Kristo." Kazi zenu zinathibitisha mnavyoamini.

235 Yesu alisema, "Ishara hizi," z-i-t-a, "zitafuatana na hao waaminio, kwenye utimilifu wa dahari. Na katika Jina Langu watatoa pepo, wanene kwa lugha mpya; kama wakishika nyoka, wala kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru. Wakiweka mikoo yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hivyo ndivyo alivyosema Yesu. Hayo ndiyo Maneno ya mwisho yaliyotoka kinywani Mwake. Ndipo akachukuliwa juu Mbinguni.

236 Nao watu wanaotoka, wakiamini na kuhubiri Kuponya Kiungu, na nguvu za Mungu, ulimwengu unawaita "wenye kichaa." Nayo Biblia ilisema, "Kama wakimwita Bwana wa yumba 'Belzebuli,' ni zaidi jinsi gani watakavyowaita, wanafunzi Wake?"

237 Kuhukumiwa, hao hapo, wote walikufa kabisa. Lakini Josephus alisema, "Watu hao watu ambao . . . Hao—hao watu wa Kikristo, walikuwa wametoka Yerusalemu wakaenda Judea, nao wakaitoroka hasira hii yote." Sasa hao walikuwa Wayahudi, kuisha kwa Wayahudi.

238 Upesi sasa, kwa dakika chache zifuatazo, hebu tumalize Mataifa, upesi sana. Hebu tufungue katika Ufunuo sura ya 7, ambapo tutamalizia majira ya Mataifa. Muone kama jambo hili ni kweli ama si kweli. Hapo ndipo nabii wa Ezekieli 9 alipohubiri mwisho wa wakati *huu;* sasa huyu hapa Roho

Mtakatifu akitabiri mwisho wa wakati *huu*. Sikilizeni kwa makini sasa ninaposoma kwa uangalifu.

> *Baada ya hayo*. . .

239 Ufunuo 7 sasa, "Baada ya mambo haya nikaona malaika wanne. . ." Hao walikuwa ni wale wapanda farasi waliotoka wakaenda, kwenye sura ya 6, na jinsi walivyokwenda; farasi wa kijivujivu, na farasi mweusi, na farasi mwekundu, na kadhalika, ambao, hao wapanda farasi walikuwa wakipanda farasi nchini kwa muda mrefu.

> . . .*nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne*. . .huo *upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wo wote.*

240 Sasa angalia lile ono aliloona kwanza. "Nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne," mahali panne kuizunguka dunia, malaika, akizizuia pepo nne. *Malaika* ni "wajumbe." Biblia ilisema jambo hilo. Halafu *pepo* ni "vita na ugomvi." Yeye alikuwa anazuia pepo nne, hapa. . .?. . .Sasa angalia, aya ya 2.

> *Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka maawio ya jua, mwenye* (m-u-h-u-r-i, kazi iliyomalizika, katika maneno mengine). . .*mwenye muhuri ya Mungu aliye hai; akawapigia kelele kwa sauti kuu*. . .*malaika*. . . ambao *waliopewa kuidhuru nchi na bahari,*
>
> *Akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya* kipaji cha uso wao.

241 Angalia, nitaendelea kusoma.

> *Nikasikia hesabu yao waliotiwa muhuri*. . .mi—mi-. . . *waliotiwa muhuri* ka-ka. . .*katika kila kabila ya—ya*. . . *kabila ya Waisraeli, watu mia na arobaini na nne elfu.*

242 "Wa kabila la Yuda, kumi na mbili. . ." na kuendelea moja kwa moja, na "Benyamini," na "Gadi," na "Reubeni," na kuendelea hata kwenye "Zabulon," na moja kwa moja hata kwenye yale makabila kumi na mawili, mwisho wa aya ya 8. Na kumi na mbili mara kumi na mbili ni ngapi? [Kusanyiko linasema, "Mia na arobaini na nne."Mh.] Mia na arobaini na nne. "Mia na arobaini na nne elfu," wote Wayahudi. Sasa, angalia.

> Na b*aada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila* jamaa, lugha, na mataifa,. . .

243 Hao walitoka wapi? Mnaona, tunaona ambapo hao Wayahudi mwishoni; na wakati wale malaika walipoamrishwa kwenda na kuangamiza, ilisema hapa ndani, waliona na

"kuzuia." Lakini hawa walitoka wapi, wa jamaa zote, lugha, na mataifa. Walijitokeza jukwaani.

> . . .*na* watu, *na lugha, wamesimama mbele za* Mwana-Kondoo, *na mbele za*. . .walikuwa *wamevikwa*. . . *Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende* mkononi *mwao;*

244 Bibi-arusi, Bibi-arusi wa Kimataifa alikuwa ametiwa muhuri hapa. Angalia.

> *Wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu* anayeketi juu ya kiti cha enzi na juu *ya Mwana-Kondoo.*

> *Na—na malaika*. . .waliokuwa *wakisimama pande zote za kile kiti cha enzi*. . .*hao wazee*,. . .*wale wenye uhai wanne*,. . .*wakaanguka kifulifuli mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujudu Mungu,*

> *Wakisema*,. . .(Sikilizeni, kama huu hausikiki kama mkutano wa Roho Mtakatifu!) Ba-. . .*Baraka*, amina; . . .*utukufu*, . . .*hekima*, . . .*shukrani*, . . . *heshima*, . . .*uweza*, . . .*nguvu, zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina.*

245 Hiyo haisikiki kama namna fulani ya ibada ya kidini ya kupandisha cheo, kwangu mimi. Hiyo inasikika kama kumwagwa kwa mtindo wa kale kwa Roho Mtakatifu, kwangu mimi. Watu hao walikuwa mahali fulani; walijua la kufanya walipomwoa Mwana-Kondoo ameketi kwenye Kiti cha Enzi.

> *Akanijibu mmoja wa wale wazee akaniambia, Je! watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? nao* wanatoka *wapi*?

246 Sasa unajua Wayahudi wote, lakini hawa walitoka wapi, "jamaa wote, lugha, na mataifa"? Angalia.

> *Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe*. Yohana akasema, "Mimi sijui." *Akaniambia*,. . .

247 Hawa ndio wale waliokuwa na jambo Hilo, nadhani. Vema.

> . . .*Hao ndio* wanatoka *katika dhiki ile iliyo kuu*, (walioitwa "watakatifu wanaojifingirisha," wakadhihakiwa, wakateswa, wakachekwa) . . . waliotoka *katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo*. (Angalia)

> . . .*wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu*,. . .

248 Mke anakaa wapi? Malkia anakaa wapi? Huyo ni Bibi-arusi, huyo Bibi-arusi wa Mataifa.

> . . .*nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake,*

249 Mke wangu hunitumikia nyumbani, usiku na mchana. Mnaona? Huyo ni Bibi-arusi wa Yesu; huyo ni Bibi-arusi wa Mataifa.

> . . .*na* hao *aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao.*
>
> Nao *hawataona njaa tena,*. . .

250 Haleluya! Siku za kazi zimekwisha. Vema, tulikosa chakula mara nyingi, lakini hatutakosa hata mara moja Kule. Amina.

251 Najua maskini mama yangu mdogo anaketi hapa usiku huu. Nami nimemwona akitoka mezani. Tulikuwa na kahawa na mkate uliooza. Yeye angeitia, akaweka sukari. Wala hakuna ya kutosha; watoto wangelia, naye angesimama akaondoka. Bali hatutafanya jambo hilo Kule! Baba yangu mzee alilalia mikono yangu, upande wa pili wa barabara, kule, akafa, ana njaa.

252 Lakini hatutafanya jambo hilo tena. Haleluya! La, bwana. Hamna njaa tena.

> Wao *hawataona njaa tena, wala* wao *kiu*. . .*wala* jua halitawaangazia,. . .
>
> *Kwa maaa huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi,* atawalisha, *naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.*

253 Huenda watalia kidogo na kupiga makele, wakati Roho Mtakatifu ajapo. Lakini Mungu atayafuta machozi yote katika macho yenu.

254 Angalia, yeye aliona "malaika wanne wamesimama katika pembe nne, wakizizuia pepo nne." Upesi sasa. Wakati wangu umekwisha, bali hebu niwaambie jambo hili, kabla ya kufunga. Angalieni, yeye aliona malaika wanne. Alioa mwisho wa kanisa la Kiyahudi, jinsi alivyowaona wakija kwa jia ile ile; wakija pamoja na silaha za kufisha, jeshi hilo.

255 Sasa angalia. Kanisa la Roho Mtakatifu lilipokea alama ya namna gani, kama alama ya kipaji cha uso? Ilikuwa alama ya kiroho. Roho Mtakatifu aliwatia alama. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye hakuchanja cho chote kichwani mwao. Sivyo? ["La."] La.

256 Wao hawakuhukumiwa na nchi fulani inayopinga dini. Walihukumiwa na yao wenyewe. Mnaona ninalomaanisha? Kanisa halisi la Mungu aliye hai litahukumiwa na Katoliki na Protestanti, maana wao wataungana. Tayari wako pamoja kama mmoja, kama mama na binti.

257 Lakini hawa, *hapa*, hawakuungana. Kisha, angalia kile Yeye alichofanya. Alisema, "Tia alama kwenye kipaji cha uso wao." Ilikuwa alama ya namna gani? Nitawasomea, Matendo

2. “Walikuwa wote mahali pamoja katika moyo mmoja. Kukaja ghafla uvumi, Malaika akishuka kutoka Mbinguni.”

Mnasema, “Hivi huyo Malaika alikuwa ule uvumi?”

258 Ilikuwa nini, ni nini kilichomtangulia Daudi, wakati aliposikia uvumi wa majani, majani ya miforsadi, ule usiku wakati aliogopa kuendelea mbele? “Alisikia sauti kutoka Mbinguni kama ya upepo wa nguvu ukienda kasi,” Mungu anawatangulia.

259 “Mara akawatokea Roho Mtakatifu na Nguvu.” Wakatoka kwenda mitaani, wakirukaruka na kuruka, na kunena kwa lugha, na kwa midomo ya kigugumizi, na kupiga makelele, na kutenda kama walevi, na kila mtu akifurahi tu na kumsifu Bwana Mungu. Hiyo ni kweli?

260 Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya anaposhusha Nguvu Zake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Naye akaingia moja kwa moja mle, nao Ujumbe ukaenea! Haleluya! Nao wakapiga makelele na kupaza sauti, na kunena kwa lugha, kisha wakatoka wakaenda kule. Basi hiyo ndiyo alama ambayo Mungu aliwatia hao watu. Sivyo? Mungu aliwatia alama, na hiyo ndiyo alama Mungu atakayowatia watu Wake leo. Muhuri ile ile ya Mungu iliyotiwa juu yao kule, chini ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, ilikuwa ndiyo Muhuri ya Mungu.

261 Nataka kuwaulizeni jambo fulani, enyi kanisa. Biblia inasema ya kwamba alama ya Mungu, katika siku hiyo, ilikuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ile alama iliyokuwa juu ya watu, kuwafanya tofauti na wengine, ilikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Agano Jipya lilisema, katika Waefeso 4:30, ya kwamba Roho Mtakatifu ndiye muhuri ya Mungu, kwa ajili ya watu katika siku za mwisho, hata kikomo chako cha Milele. Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Basi Roho Mtakatifu alikuwa kweli.

262 Naam, tulikuwa na wakati wa Kimethodisti, tulikuwa na wakati wa Kibatisti, tulikuwa na kuhesabiwa haki, tulikuwa na kutakaswa. Tulikuwa na mambo haya yote, yakija.

263 Halafu yapata miaka arobaini iliyopita, ubatizo wa Roho Mtakatifu ulijulikana Marekani. Hiyo ni kweli? Yapata miaka arobaini iliyopita, wakati watu walipoanza kupokea . . .

264 Naam, walizoea kuuita kazi ya pili dhahiri ya neema, utakaso. “Utakaso,” ni kweli.

265 Chombo hakina budi kuchukuliwa kwanza, kuokotwa. Kimejaa matope. Kimehesbiwa haki, kwa maana yu—yule mtu alikitwaa.

266 Jambo la pili ni, hakina budi ku—kusafishwa na kusuguliwa. Neno *kutakasa* linamaanisha “kusafishwa, na kutengwa kwa ajili ya matumizi.” Lakini “kutengwa *kwa ajili* ya matumizi” haimaanishi kwamba *unatumika*.

267 Ndipo Yesu akasema, "Heri ninyi mnapopata njaa na kiu ya haki, maana mtashibishwa." Mnaona, Roho Mtakatifu alikuja juu ya mwamini aliyetakaswa, aliye halisi, wa kweli. Nazo ishara na maajabu zikaanza kujidhihirisha zenyewe mara chombo hicho kilichotakaswa kilipokuwa sawa, na Roho Mtakatifu akaingia mle. Mnaona ninalomaanisha?

268 Huwezi kutoa mafuta kutoka kwenye chupa hiyo isipokuwa kuwe na mafuta mle, haidhuru hiyo chupa ni safi namna gani. Huwezi kuleta kunena kwa lugha, a kuponya Kiungu, na Nguvu za Mungu, kutoka kwenye kitu kitupu. Ilimbidi Roho Mtakatifu kuletwa, basi.

269 Angalia, yapata miaka arobaini iliyopita . . . Hebu tukumbuke. Tunaangalia, kila mahali . . . Angalieni kwa makini. Kuna mtawala mkuu aliyejitokeza, wa Vita vya Kwanza vya Dunia; mara ya kwanza katika historia ya ulimwengu mzima, vita vya dunia. Alikua anaelekea wapi? Moja kwa moja katika Ujerumani. Nini kilitokea? Mabadiliko; hakuna ajuaye, hata wa leo, jinsi vilivyomalizika. Hakuna anayejua. Someni katika *Kumalizika Kwa Vita vya Dunia*. Kila kitabu, nimekisoma. Hakuna mtu hata mmoja . . . Jambo pekee wanalojua, kulitokea amri, "Jisalimisheni!" Hakuna anayejua ni nani aliyetoa hiyo amri. Kwa nini?

270 Ee Mungu! Mtaniita "mtakatifu anayejifingirisha," haidhuru, kwa hiyo afadhali nitende ninavyojisikia. Angalia! Jinsi ninavyoshukuru kwa ajili ya Roho Mtakatifu kuwa hapa kwenye jukwaa, kufunua.

271 Angalia. Tazama. Walitoka wakaenda, kila upepo ukija ulimwenguni, silaha za kisasa, kuangamiza kila kitu katika vita vya dunia. Lakini, kwa ghafla, vikakoma. Ufunuo sura ya 7, ilisema, "Nikaona malaika saba wakishuka pamoja na silaha za kufisha. Na kulikuwako na Mtu aliyetoka kwenye Maawio ya Jua, mwenye muhuri ya Mungu aliye hai; kasema, "Zizuieni pepo nne!"

272 "Zizuieni," kwa nini? Wayahudi hawako mahali panapofaa bado. Utukufu! Wayahudi hawako mahali panapofaa, kama alivyoahidi Mungu. Yeye aliwaambia mahali watakapokuwa, watakakosimama kule. Alisema, "Mtakapoona mtini ukichanua majani, jueni wakati umekaribia." Na mtakapoona Wayahudi wakirudi Palestina, jueni wakati umekaribia. Kizazi hiki hakitapita mpaka mambo yote yatakapotimia." Basi, ndugu, miaka saba iliyopita ndio wakati wa kwaza ambapo bendera ya Wayahudi imepata kupepea, katika miaka elfu mbili, juu ya Yerusalemu; naam, miaka elfu mbili mia tano. Amina. Wayahudi hawakuwa mahali ambapo jambo hilo lingetendwa, lakini Yeye alisema, "Zizuieni! Zizuieni!"

273 Kwa nini, kwa nini "kuzizuia"? Angalieni, kulikuwako na Mataifa fulani bado, kati ya wakati wa Wesley na wakati

wa Pentekoste, iliwabidi kuingia. Kabla ya Wapentekoste kuingia katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, kulikuwa na "mlango uliofunguliwa" uliowekwa mbele ya kanisa; mlango ulifunguliwa, kwa, "Yeye atakaye na aje anywe katika Chemchemi ya maji ya Uzima bure." Mlango uliofunguliwa, uliwekwa. Loo, jamani!

Kisha Yeye akasema, "Zizuieni!" Kwa nini?

274 Yesu alisema, "Mtu fulani alitoka kwenda kufanya kazi. Kisha mwingine akaondoka akaenda, katika saa nyingine, akafanya kazi. Mtu mwingine akaondoka akaenda akafanya kazi. Na mtu mmoja aliondoka akaenda saa kumi na moja. Basi aliposimama saa kumi na moja, alimpa kila mmoja wao sehemu ile ile, saa kumi na moja. Hao wakashangaa mbona hivi. Mbona yeye, alipata saa kumi na moja, kila mtu akiingia?

275 Wale wa Martin Luther waliofanya kazi, walitembea chini ya majira ya Luther, wakafa katika neema!. . .?. . . wengine, Wamethodisti waliopiga makelele, ambao walikufa chini ya Wakati wa Wesley, walikufa katika neema. Tunaishi katika wakati mwingine, si kule nyuma. Hapa! Mama alikuwa anasafiri kwa gari la ng'ombe, nasi tunasafiri katika Ford muundo wa V-8, karibu kuendeshwa kwa ndege. Hiyo ni kweli. Tunaishi katika wakati tofauti, kwa jumla. Pia tunaishi katika majira tofauti. Tunaishi katika siku za kurudishwa kwa Nguvu za Mungu, na papa hapa tunaona nguvu za Mungu kama walivyofanya hapo mwanzo. Tunaishi katika wakati mwingine. Msiangalie nyuma kwenye Wesley, Methodisti, na hao wote, Batisti, na Presbiteri. Angalieni hapa kwa Yesu Kristo, Mwanzilishi na Mwenye Kukamilisha Imani ya Biblia. Haleluya!

276 Sasa mwagalie Yeye, kasema, "Zizuilieni," hata (lini?) watu wa saa kumi na moja waingie, kule kuitwa kwa mwisho kwa Mataifa. Mama alifanya kazi *kule*; baba na hao wengine walifanya kazi *hapa*; nyanya alifanya kazi *kule*. Huu ni wakati wetu, saa kumi na moja. Hivyo Vita vya Dunia vilikwisha katika mwezi wa kumi na moja mwakani, siku ya kumi na moja ya mwezi, saa kumi na moja ya siku, na dakika ya kumi na moja katika hiyo saa; ili kwamba watu wa saa kumi na moja wapate kuingia, (kwa nini?) wapate ubatizo ule ule wa Roho Mtakatifu walioupata nyuma *hapa* hapo mwanzo, kurudisha Nguvu za kufufuka kwa Bwana Yesu Kristo, ishara zile zile na maajabu.

277 Ni kitu gani? Vita viking'ang'ana *hapa* viking'ang'ana *pale*; viking'ang'ana *hapa*, viking'ang'ana *pale*; vikijaribu ku-. . . Mbonu za atomiki na cho chote kile zinaundwa, bali hazitafanya jambo hilo. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara kadha—Mh.] Haziwezi kufanya jambo hilo mpaka Wayahudi watakapopata kuzuriwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Malaika alisema, "Zizuilieni, hata tutakapowatia hao watumishi muhuri," si Bibi-arusi. Mataifa kamwe hawajakuwa watumishi;

sisi ni wana na binti. Hao ndio watumishi, Wayahudi. Ibrahimu alikuwa mtumishi wa Mungu. Haleluiya! Sasa, tunaona maelfu mara maelfu ya Wayahudi. Mungu aliufanya mgumu moyo wa Farao, apate kuwafukuza waende Palestina. Mungu aliufanya mgumu moyo wa Hitler, moyo wa Mussolini, moyo wa Stalin. Yeye anawafukuza kwa nguvu, mpaka Palestina, bila kujua analofanya, akitenda kazi moja kwa moja katika mikono ya Mungu.

278 Halafu wale mia na arobaini na nne elfu watasimama kule. Na moja ya siku hizi, nabii fulani wa Kiungu, mtakatifu, mtiwa mafuta wa Mungu ataenda kule akiwa na ishara na maajabu. Hao Wayahudi watasema, "Hilo ndilo ninalotazamia." [Ndugu Branham anagonga mimbara mara nne—Mh.] Naam, bwana. Ndipo Mungu atawabatiza Wayahudi mia na arobaini na nne elfu.

279 Ndipo Kunyakuliwa kutakuja; wakati wa Mataifa utakwisha. Mbomu la atomiki litalipuka liuchukue ulimwengu. Nalo Kanisa la Kimataifa litanyakuliwa juu, likasimame pale katika Uwepo wa Mungu. "Ni nani hao wanaotoka katika ile dhiki iliyo kuu? Wameosha mavazi yao katika Damu ya Mwana-Kondoo. Wao wako mbele za Mungu, bila waa." Amina.

280 Alama ya mnyama, muungano; makanisa, Ukatoliki, yote yameungana, yataingia katika machafuko. Masalio, Bibi-arusi wa Roho Mtakatifu.

281 Nao watu leo ambao wanacheka kunena kwa lugha, ambao wanacheka kupoya Kiungu, wanaocheka unabii, wanacheka dhihirisho la Roho; na roho ile ile iliyowatawala wale Wayahudi hapa nyuma, ambao walimkufuru Roho Mtakatifu kule nyuma, kisha wakafa chini ya hukumu ya Kiungu. Marekani hii iko chini ya hukumu ya Kiungu, chini ya Nguvu za Roho Mtakatifu. Wametuhukumu, na kutufanyia mzaha, na kutufukuza, na kutuita "watakatifu waaojifingirisha" na cho chote kile. Bali saa imewadia, ambapo Mungu atamwaga hukumu Yake ya Kiungu. Amina.

282 Iweni tayari. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . .?. . . Mahali pa salama pekee leo ni katika Kristo Yesu. Mungu awabariki. Iwapo huko ndani, jitahidi mpaka uingie. "Hao walio katika Yesu Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye katika Kuja kwa Pili."

283 Bila muhuri ya Mungu, ambayo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, muungano wa ukengeufu ndio alama ya mnyama. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaona ninalomaanisha? Lakini hawa waalimu wa kidini wanajaribu kuweka jambo hilo katika ukomunisti, huku hawatambui kitu hicho kinatenda kazi moja kwa moja kati yao. Yeye alisema, "Watakuwa viongozi vipofu wa vipofu." Alisema, watakuwa na macho, bali hawawezi kuona." Kasema, "Enyi, na katika mapokeo yenu, mnanena fundisho

la wanadamu, mnafanya maagizo ya wanadamu, mkiyafanya maagizo ya Mungu bure."

284 Mtacheka Katoliki kwa kuitengeneza katekismo yao, nao watu wenu wanaenda moja kwa moja hapa kwenye mkutano fulani ama cho chote kile, na kuamua kama wanaweza kupokea kuponya Kiungu, ama ubatizo wa Roho, na mambo haya. Nao wanalihukumu na kulikataa. Nanyi mnacheka Katoliki. Hamna haki yo yote ya kucheka Katoliki. Maana, kama alikuwa "KAHABA," Biblia ilisema wewe ni "MALAYA," katika muungano ule ule.

285 "Tokeni kwake, enyi watu Wangu! Makatengwe nao," asema Mungu, "nami nitawapokea Kwangu." Hiyo ni kweli.

286 Loo, mbona haya Maskani ya Branham hawashiki shauri la kufaa? Nataka kujua kama ninyi watu mlio hapa mnaamini Injili hii. Nayo imehubiriwa, nanyi mmeiona Hiyo, ishara na maajabu, na kuthibitishwa. Na kila kitu ambacho Bwana amenena, kimetimia. Basi, kuna nini huku, ninaposikia kuna ugomvi kati yenu, ninaposikia kuna ubishi? Ninataka muandike kuna nini kwenu, yale yaliyo moyoni mwenu, na kuyaweka kwenye jukwaa hili la mimbara, kesho usiku. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.]

287 Nataka kuona kwa nini kanisa hili haliwezi kubebwa na Nguvu za Mungu, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na ishara na maajabu. Kuna nini? Mchungaji wenu analiamini Hili. Mnaliamini. Kwa hiyo, kuna nini hapa? Kuna kasoro. Haya yanapaswa kuwa ndiyo mnara wenye taa wa ulimwengu. Haya yanapaswa kuwa ni mahali ambapo Nguvu za Mungu, na kuomboleza na kulia, na kumtafuta Mungu, kunapaswa kuwa kunaendelea, usiku na mchana. Mbona hatuwezi kuwa na jambo hilo?

288 "Nataka, bali ninyi hamtaki," akasema Yesu. "Msingetaka. Njoni mkanunue Kwangu."

289 "Najua mnasema," Yeye akasema, "ninyi ni 'tajiri, hamna haja na kitu,'" akizungumza na makanisa. Kasema, "Mnasema, 'Mimi ni tajiri, na sina haja na kitu. Sisi ni madhehebu makubwa zaidi.' Wala hamjui, bali ninyi ni wanyonge, maskini, wenye mashaka, vipofu, na uchi, wala hamjui." Kama mtu yuko katika hali kama hiyo na anajua, atajisaidia mwenyewe. Lakini, unapokuwa namna hiyo, "wala hujui!" Naye Kristo alisema makanisa katika siku hii yangekuwa namna hiyo, wala yasingejua jambo hilo.

290 Finya utu wako wa rohoni, ndugu yangu mpendwa, mpendwa sana. Finya nafsi yako, kama tusemavyo, kwa maombi, na kusema, "Bwana Yesu, nichunguze. Jalia nifanye hesabu usiku huu, kabla sijaenda kitandani, nione kuna nini kwangu. Nimekuwa nikikiri kwa miaka kadha, nami sioni vitu hivi alivyosema Yesu. Ya kwamba Yeye angekuwa pamoja nami,

na mambo haya yangeendelea, sioni jambo hilo. Kuna nini, Bwana Yesu?”

291 Iweni waaminifu. Iweni wanyenyekevu. Shukeni mje mkazungumze naye, kama vile uso kwa uso na ndugu. Yeye atawafunulia. Atawaambia. Atairarua nafsi yako vipande-vipande, na kuiweka huko. Semeni, “Bwana Yesu, kama jambo hilo likinigharimu jamaa yangu, kama likinigharimu maisha yangu, kama likinigharimu kazi yangu, kama likinigharimu ushirika wangu, kama likinigharimu sifa zangu mjini, nitashika njia pamoja na wachache wa Bwana wanaodharauliwa.”

292 Sasa kumbukeni, Yesu alisema, “Mlango ni mwembamba, na njia imepanda, bali lakini ni wachache watakaoiona. Kwa maana njia ni pana inayoongoza kwenye uharibifu.” Milioni moja zaidi katika ’54, “Njia ni pana iendayo upotevuni, na ni wengi wanaoipitia. Hiyo ni kweli. “Yeye atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili Yangu atayapata.” Yeye anayempenda baba, mama, dada, ndugu, wala cho chote, zaidi ya Mimi, hastahili kuitwa Wangu. Atatia mkono Wake kweye jembe na kuanza kusonga mbele, hata akigeuka nyuma, yeye haustahili huu wakati.” Ndugu!

293 Moja ya siku hizi, mahubiri ya mwisho ya Injili iliyotiwa mafuta na Roho Mtakatifu yatahubiriwa. Moja ya siku hizi, bunduki ya mwisho itapigwa. Moja ya siku hizi, wimbo wa mwisho utaimbwa. Moja ya siku hizi, ombi la mwisho litaombwa. Moja ya siku hizi, milango ya haya maskani itafungwa kwa mara ya mwisho, Biblia itafungwa mimbarani. Nanyi mtasimama Mbele ya Mungu, kutoa hesabu kwa ajili ya yale mliyosikia usiku wa leo. Vipi basi? Vipi basi? Hapo kile Kitabu kikubwa kitakapofunguliwa, vipi basi? Wakati usiku wa leo unapokuja kwenye rekodi, vipi basi? Loo, kama wimbo unavyosema:

> Vipi basi?
> Hapo kile Kitabu kikubwa kitakapofunguliwa,
> vipi basi?
> Hapo wale ambao wamemkataa Mwokozi leo,
> Wataulizwa kutoa sababu, vipi basi?

294 Kazi yako ilikuzuia. Wazazi wako walikuzuia. Mpenzi wako wa kiume alikuzuia. Mpenzi wako wa kike alikuzuia. Kanisa lako lilikuzuia.

> Vipi basi? Vipi basi?
> Hapo kile Kitabu kikubwa kitakapofunguliwa,
> vipi basi?
> Hapo wale ambao wanaoukataa Ujumbe huu
> usiku wa leo,
> Utau-. . .utaulizwa kutoa sababu, vipi basi?

295 Utafanya nini juu ya jambo hilo? Unajua alama ya mnyama ni nini. Unajua muhuri ya Mungu ni nini. Ni juu yako.

Bwana na awabariki, tunaposimama.

296 Ewe, Baba wa Mbinguni, jalia huruma Zako na baraka ziwe juu ya watu. Jalia Roho Wako atende kazi. Na jalia Roho Wako Mtakatifu awajilie watu hawa, na awape, Bwana, ubatizo wa Roho. Jalia kila mwanamume na mwanamke, mvulana na msichana, humu ndani, na wachukuliwe sana usiku wa leo, na Roho Mtakatifu, hata watasema, "Mungu, chukua yote niliyo nayo. Chukua kila kitu nilicho mimi. Lakini, naomba nikutumikie Wewe, Bwana wangu. Nitaweka kando kila kitu. Nitatoa nafsi yangu. Nitaacha kiburi changu. Nitaacha kanisa langu. Nitatoa kila kitu."

297 Si kwamba ingewabidi kutoka katika kanisa lao, Bwana, bali hawana budi kutoka katika hali wanayoishi. Ee Mungu, watume Wamethodisti warudi katika kanisa lao, wameshika moto, kuhubiri Injili; warudishe Wabatisti, warudishe Wakampbelli, warudishe Wakatoliki. Bwana Mungu, mtume mtu fulani kutoka kwenye Maskani ya Branham hapa, arudi maskanini humu, akiwa na roho mtiifu na mnyenyekevu, ambaye atatoka aende na kunena, na kupenda, na kujaribu kuwaleta watu katika umoja tena, ili kwamba Roho Mtakatifu aweze kuingia na kuwatumia watu. Tuma ishara kubwa na maajabu. Mtie mafuta kila mwamini. Samehe kila dhambi.

298 Ee Mungu, tunaona ishara zikija. Tunaona mtini ukichanua majani. Tunajua ya kwamba wakati umekaribia. Tunaona zile mbomu zimewekwa kule ng'ambo katika mikono ya yule mtu uliyesema ameamrishwa kuuangamiza ulimwengu.

299 Ee Mungu, tunawezaje kukataa tena? Tunawezaje? Wakati, tunaisikia Injili Yako iliyobarikiwa ikitangazwa dhahiri sana, dhahiri; tunamsikia Roho Mtakatifu akiongoza; tunamwona Roho Mtakatifu akitoa ishara na maajabu; akiwaponya wagonjwa, akiyafungua macho ya vipofu, akiurudisha uhai wa waliokufa; maajabu makuu pamoja na ishara; Injili ikihubiriwa na wasiojua kusoma, watu wajinga, ikihubiriwa chini ya Nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu; ishara na maajabu zikilifuata kanisa. Ni kiasi gani tena!

300 Wewe ulisema, "Kama mngalimjua Musa, mngaliijua siku Yangu." Haleluya! Vivyo hivyo leo, Bwana. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara tatu.] Wao wanaona kila namna ya ishara, za vita na shida, na kila kitu. Wajalie wageuze kurasa za Biblia ya kale yenye thamani, waone mahali ilipo ile nguzo ya kupimia urefu. Tuko kwenye mwisho wa wakati.

301 Ee Mungu, peleka Roho Wako juu ya watu hawa. Na wanapoondoka kutoka hapa, usiku wa leo, Roho Mtakatifu na aende pamoja nao.

302 Na kesho usiku, Bwana, tutakaposhuka kuja kwenye mwito huu wa madhabahu tunaojiandaa kutoa, tunaomba ya kwamba madhabahu yatajazwa kabisa, vyumba vya maombi vitajaa.

303 Tena naomba, Jumapili asubuhi, Bwana, na Jumapili usiku, tutakuwa tukiwabatiza watu hapa kulingana na Neno la Mungu. Pia naomba Roho Mtakatifu awe anashuka juu ya maji hayo, na kufanya ishara kuu na maajabu. Jalia jambo hilo, Baba.

304 Mbariki mchungji wetu mpendwa. Wabariki washiriki. Wabariki wageni kwenye malango yetu. Naomba twende nyumbani usiku wa leo na kuyawazia mambo haya moyoni mwetu; turudi kesho usiku, tukifurahi, tukileta miganda. Tuaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

305 Bwana Yesu Kristo ambariki kila mmoja wenu. Peaneni mikono. Rudini kesho usiku, mkileta mahitaji yenu na kile mnachotaka, mkayaweke mimbarani. Mungu na awatie mafuta daima, awe pamoja nanyi! Amina. Mungu awabariki.

Muhuri Ya Mungu SWA54-0514

(The Seal Of God)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, 14 Mei, 1954, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1994 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org